KANISA NI NINI?

Madhumuni ya somo hili :

Somo hili limetungwa ili kusaidia kikundi cha waamini jinsi Mungu alivyo lianzisha na pia kulikuza Kanisa lake baada ya kufa na kufufuka kwa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Mafundisho haya pia yatasaidia kumwonyesha msomaji mienendo na makusudi na makusudi makuu ya kanisa la Agano Jipya . Baada ya kumaliza somo, matumaini yetu ni kwamba kikundi cha waamini wataweza kutumia kanuni hizi ili kuanzisha walau Kanisa moja la Agano Jipya lenye afya.

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa uinjilisti wa Kigunduzi ulioandaliwa kwa ajili ya ufuasi katika uanzishaji wa makanisa na ufuasi uitwao “Habari njema za Yesu Kristo” na “ Kuanza Maisha mapya katika Kristo!

Jinsi ya kutumia mwongozo huu :

1. Mwongozo huu utatumika katika kikundi cha watu ambao wengi wao wamekwisha kata shauri kumwamini Kristo. Kiongozi atajaribu kuwasaidia waamini hawa waanzishe hata kanisa moja katika eneo . Bwana angewaongoza kuanzisha makanisa kadhaa. Ikiwa wengi katika kundi hawajakata shauri kumwamini Kristo, wanaweza kuongozwa katika mafundisho ya Biblia ya Uinjilisti wa kiuvumbuzi kama vile “Habari njema za Yesu” kilichoandikwa na Christy Brawner, au “Habari Njema kwako” kilichoandikwa na Charles Brolck.

Kama wapo wakristo wapya ni muhimu na msaada daima kuwaingiza katika mafunzo ya ufuasi kama vile “ kuanza Maisha mapya katika Kristo “ yaliyotungwa na Christy Brawner; “Kweli sita kwa waumini wapya” kilichoandikwa na wade Akins. Hili litawasaidia kuwa na mizizi katika misingi ya kanuni za Imani.

2. Kwanza, kukusanya kikundi cha watu pamoja kujifunza “Kaniani ni nini ?” Hakuna idadi ya watu iliyopangwa ili kushiriki katika fundisho hili. Anza kila somo na muda wa Ushirika na maongezi . Kumbuka kuwa kanisani ni mahali pa kuunda familia. Familia zinahitaji kucheka, kulia na kuomba pamoja. Anza kila somo na muda

huu wa maongezi katika kundi ili waweze kujenga urafiki na watu wasiowafahamu bado.

3. Baada ya maongezi, tumia dakika chache katika kuombea mahitaji ya kila mmoja, mshukuru Bwana kwa jinsi alivyo na kwa yale aliyowatendea na ombea maendeleo ya kanisa hili mnalotaka kuanzisha. Baada ya maombi, Chukuaeni muda katika kuimba nyimbo chache za kumsifu Mungu na kutoa shuhuda kwa yale ambayo Mungu anayafanya katika maisha yenu. Huenda pengine mkaanza kujizoeza kutoa fungu la kumi kwa Kanisa.

4. Anza somo la kwanza kwa kusoma simulizi za hadithi. Kiongozi anaweza kusoma hadithi au anaweza liwaruhusu wanakikundi wasome aya moja moja. Kiongozi arudie kuisimulia hadithi kwa maneno yake mwenyewe ili ieleweke zaidi. Baada ya juma la kwanza, kutakuwa na maswali ya marudio kuhusu hadithi za wiki zilizotangulia.

5. Liongoze kundi katika kupitia maswali yote ya mjadala. Kusudi la maswali ni kusaidia kakaza hatua kwa hatua yale yaliyotokea katika sura hizo ndani ya Biblia.

6.Soma kweli zote za Kiroho. Kweli za kiroho ni mienendo ya muhimu tunayojifunza kuhusu Mungu, sisi wenyewe na kanisa lake kutoka katika maandiko. Waruhusu wanakikundi kueleza fikra zao kwa kila kweli ya kiroho. Kanisa lako litakuwa linakata shauri kwa kujitambua ni nini ndani ya majuma machache yajayo. Waongeze kuangalia sura ndani ya Biblia zilizo orodheshwa wakati wa Juma ili ziaksi zaidi kwa yale waliyojifunza.

7. Funga kila kikundi kwa sala ukitumia muda kutafakari uliyojifunza. Msihi kila mtu aende nyumbani na kusoma sura hiyo katika biblia.Ni biblia tu ndiyo itakayo kuwa msingi wa uelewa kuhusu kanisa.

8. La mwisho na la muhimu zaidi, anza kutumia yale uliyojifunza kwa kuanzisha makanisa zaidi kwa ajili ya ufalme wa Mungu.

Matendo 1 – 13

Somo 1 – Roho mtakatifu anaahidiwa (ahadi ya Mungu kwetu leo na sala) – Mdo 1
Somo 2 - Kanisa laanza (Ushauri na Idada) – Mdo 2.
Somo 3 - Huduma ya Kanisa yapanuka (Huduma) Mdo 3-4
Somo 4 – Kanisa lashambuliwa kutoka ndani (ufuasi) Mdo 4-5
Somo 5- Kanida lashambuliwa kutoka nje (Uwakilishi,Mateso) Mdo 6
Somo 6- Viongozi wa Kanisa waeneze neno (Ubatizo na meza ya Bwana) mdo 8.
Somo 7 – Mmishenari mkuu wa Kanisa aokolewa (Uinjilisti) Mdo 9
Somo 8 – Kanisa lapata maono kwa ulimwengu (Umisheni) Mdo 10 -13

SOMO LA 1

Roho Mtakatifu anahidiwa
(ahadi ya Mungu kwetu leo na maombi)
Matendo ya Mitume sura 1.

Kifungu kikuu "Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wagu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na samaria, na hata mwisho wan chi".

Luka, mmoja wapo wa wafuasi wa Kristo aliongozwa na Roho Mtakatifu kuandika kitabu cha Matendo. Luka anawaambia wasomaji wake kwamba katika kitabu chake cha kwanza (Injili ya Luka) alieleza yote ambayo Kristo aliyafanya mpaka muda alipopaa mbinguni . Baada ya Yesu kusulubiwa alifufuka kutoka kaburini na kwa siku arobaini alijidhihirisha kwa mitume wake. Katika muda huu, alieleza mambo mengi kuhusu ufalme wa Mungu. Yesu aliwaambia waingoje Ahadi ya Baba kwao. Ahadi hiyo alikuwa Roho Mtakatifu. Kristo aliwaambia kuwa "kweli Yohana aliwabatiza kwa maji, lakini mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu katika siku hizo chache tangu sasa" .Wanafunzi walitaka kufahamu iwapo huu ulikuwa wakati ambao Yesu angefanya mambo makuu kwa taifa lao Israeli.

Kristo alijibu kwamba haukuwa wajibu wao kujua jibu la swali hili badala yaek walipaswa kumngojea Roho Mtakatifu ili wawe "mashaidi wangu katika Yerusalemu na Uyahudi wote na samaria na hata Mwisho wan chi."

Baada ya Kristo kusema hayo, wingu likamchukua juu mbinguni. Wanafunzi wake walipokuwa wakimtazama, malaika wawili walikuja na kuwauliza kwa nini walikuwa wakiangalia juu mbinguni. Waliwaeleza kuwa siku moja Kristo atarudi tena hapa duniani jinsi hiyo hiyo kama alivyoenda mbinguni.

Baada ya hapo wanafunzi wote: Petro, Yakobo, Yohana, Andrea, Filipo, Thomaso, Barthomayo, Mathay, Yakobo "mdogo" Simon zelote na Yuda mwana wa Yakobo walienda Orofani huko Yerusalemu walikokuwa wanaishi. Huko wanafunzi waliomba pamoja. Ndugu zake Yesu walikuwa walikuwapo pia pamoja na wanawake wengi pamoja na Mariamu mama yake Yesu.

Baadaye mtume Petro akasimama na kuanza kusema na kundi juu ya kuijaza nafasi ya yuda Iskariote. Petro aliwaeleza jinsi Yuda hapo mwanzo alivyo kuwa sehemu yao katika kundi lakini alimsaliti Kristo

na kujinyonga baadaye. Alipojininginiza, mwili wake ulianguka chini na kupasuka. Konde ambako tendo la kujinyonga lilifanyika liliitwa " Konde la Damu" Hata leo.

Petro alielezea jinsi walivyo paswa kuweka mtu mwingine mahalipa nafsi ya Yuda. Walihitaji kupata mwanaume aliyekuwa pamoja tangu mwanzo wa huduma ya ubatizo wa Yohana Mbatizaji mpaka wakati wa ufufuo wa Kristo. Waliazimia kuwa watu wawili, Mathiya na Barnsaba walifaa kuwa Mitume. Wakamwomba Mungu wote ili awaonyeshe yule atakayechaguliwa. Kisha wakapiga kura zao na Mathiya akachaguliwa kuwa mmoja wa Mitume.

Maswali ya Mdomo:

1. Mtu yupi aliyeandakia kitabu cha Matendo?Ni nani aliyemwongoza ?
2. Kristo alijionyesha kwa wanafunzi wake kwa siku ngapi?
3. Ahadi ya Mungu kwetu ni nani?
4. Tunapaswa kuwa mashahidi wapi?(Kristo aliorodhesha sehemu 4)
5. Kristo aliendaje mbinguni? Atarudije?
6. Ni nani waliokutana huko orofani?
7. Nani aliwekwa mahali pa Yuda Iskariote?.

Kweli za Kiroho.

1. Mungu amemtuma Roho Mtakatifu kwetu siku hizi (Mdo 1:5)

Kristo alikuja duniani kama dhabihu kwa ajili ya dhamba zetu.Alikufa msalabani na baada ya siku tatu alifufuka kutoka kaburini. Na sasa yu Hai na yu hai na yuko mkono wa kuume wa Mungu Baba kama wakili wetu (1Yoh.2:2) Kristo aliahidi kwamba atakapoondoka duniani angemtuma Roho mtakatifu kwetu. Roho Mtakatifu ni Nani? Roho Mtakatifu ni nafsi moja katika Utatu wa Mungu . Yupo Mungu baba, Mungu Mwana (Yesu) na Mungu Roho Mtakatifu. Wote watatu ni mmoja ya yuleyule, lakini wote watatu wako tofauti na makusudi tofauti, huduma na utu wao. Biblia inatufundisha kwamba Roho Mtakatifu ana huduma nyingi ndani kanisa yeye ambaye hushuhudia (au ueleza) habari za Mungu. Yeye ni msaidizi na mshauri wetu. Vilevile huuonyesha ulimwengu dhambi yao, hitaji la haki na hukumu. Hutupatia sisi waamini vitu vizuri kama vile upendo wa kweli, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, utu wema, uaminifu, upole na kiasi.

Pia hutufanya upya kiroho, hutupa uhakika wa wokovu wetu, na hutupa karama za kiroho kwaajili ya kufanya huduma. Mafunzo haya yatafundisha kuhusu huduma za karama za kiroho katika somo lijalo. Unapoanza kujadili mchakato wa kuanzisha kanisa lako, Kumbuka kuwa utahitaji hekima nyingi kuanzisha mpango huu. Mwombe amwachilie Roho Mtakatifu awe kiongozi wakokatika yote uyafanyayo na uyasemayo. Baada ya yote, alimtuma kwetu kwa kusudi hilo.

2. **KUSUDI LA KWANZA LA KANISA NI MAOMBI (MDO.1:14)**
Baada ya wanafunzi kuona Bwana wao akichukuliwa juu mbinguni hawakutawanyika au kukimbia na kuchanganyikiwa. Walikaa pamoja, wakangoja na kuomba. Walianza huduma yao kwa njia iliyo sahihi. Walitaka kuzungumza na Mungu na kujifunza wafanye nini kifuatacho.

Ni kweli kwamba walikuwa wakiomba wakati wa huduma ya Kristo (Luka 11:2) sasa walikuwa wakiweka maombi katika matendo walipokuwa wakimngoja Roho Mtakatifu. MAOMBI ni kusudi la kwanza kanisa ambalo somo hili litachunguza.

Maombi ni njia yetu ya kuwasiliana na Baba kupitia kwa Yesu Kristo (1Tim.2:5) watu wengi wamesema kwamba Biblia ni njia ya Mungu kusema nasi, lakini maombi ni njia yetu ya kuzungumza na Mung. Katika masomo ya awali ya Uinjilisti wa uvumbuzi, pengine utakuwa umejifunza mambo matano ya kufanya katika maombi:

Omba – Omba Mungu akusaidie kwa mahitaji ya kila siku.

Shukuru – Shukuru Mungu kwa aliyokutendea wewe au wengine.
Sifu – Mpe Mungu utukufu kwa vile alivyo.

Tafuta msamaha – Mwombe Mungu akusamehe dhambi zako za kila siku

Ombea – Chukua muda katika kuwaombea kwa Mungu kuhusu mahitaji yao.

Kwa ninyi mliokwisha kumwamini Kristo, miongozo hii ya maombi inapaswa iwe sehemu ya maombi yenu ya kila siku ya maisha yenu. Hata hivyo, uanzapo kuangalia katika kuanzisha Kanisa, hautaomba kipekee, bali kama kundi. Kuna nguvu maalum katika maombi ya pamoja. Kama Kristo alivyosema,.

“ Walipo wawili au watatu wakusanyikapo kwa jina langu, na mimi nipo katika yao” (mathayo 18:20) Kumbuka kwamba Kristo alipofundisha wanafunzi wake kuomba, aliwafundisha kuomba kama kundi. Awali ya yote, alianza sala ya Bwana kwa maneno “Baba yetu aliye mbinguni” (Mathayo 6:9) badala ya kufikiria kipekee kuhusu Baba, aliwataka wawe na mtazamo wa jinsi anavyo jihusisha na kundi.

Fikiria kuhusu jinsi ninyi kama kundi mnapoweza kuja pamoja kwa maombi. Mtakutana lini? Mambo gani muhimu mtaombea? Chukueni muda muda Fulani katika mwisho wa somo hili kufikiria juu ya

maombi ya ndani sana kwa ajili yenu na kwa wengine. Maombi yangepaswa kuwa kiunganishi ya makusudi mengine, Ushirika ibada, huduma, ufuasi, uinjilisti na umisheni.

3. Ni muhimu daima kutafuta viongozi wapya (mdo. 1:26)
Yuda alichukuwa miongoni mwa wanafunzi. Huenda pengine alikuwa mwanafunzi aliye heshimiwa sana katika huduma ya Kristo pamoja na wafuasi wake. Baada ya yote, alikuwa mwanafunzi aliyekuwa mtunzaji wa fedha za huduma (Yoha. 12:6) usingeweza kumweka mtu kutunza pesa.

Pasipo kuwa na kiwango cha juu cha heshima. Kumpoteza Yuda pengine ilikuwa hasara ya maumivu makali.

Mojawapo ya vipengele muhimu katika kanisa la Agano Jipya ni kazi ya kutafuta viongozi wapya. Yuda alipomsaliti Kristo ilikuwa muhimu kutafuta mtu mwingine kujaza nafasi yake ya uongozi. Kadri kanisa lako linapoendelea kukua, utaona hitaji la kupata viongozi wapya. Kwa mfano, mtu Fulani anaweza anaweza kuhama, mnaweza kutaka kuanzisha kanisa jipya au pengine kanisa lenu linaweza kuongezeka na kwa wakati ule ule mkahitaji viongozi katika maeneo mpaya. Anza kumwomba Mungu sasa ili awaonyeshe ni watu wapi atakao wainua kuchukua nafasi kadha wa kadha za uongozi katika Kanisa lako.

Jambo la kuangalia ni kwamba , chunguza wanafunzi wa Yesu waliruhusu maombi kuongoza maamuzi yao. Katika habari hii unaona walitumia pia “kura” katika kuamua. Haya si maandiko katika Biblia ya kuruhusu kucheza kamari. Huu ulikuwa wakati wa mwisho kwa kura kutumika katika kusiaidia kutoa uamuzi. Baada ya kuja kwa Roho Mtakatifu katika Matendo 2, wanafunzi hawakutumia kura za aina hii tena.

Katika somo lijalo, tutaona jinsi Roho Mtakatifu alivyoanza huduma yake na jinsi alivyo lileta Kanisa ulimwenguni.

SOMO LA 2

KANISA LAANZA
(USHIRIKA NA IBADA)
Matendo 2.

Kifungu Kiku: "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" Md.2:38.

MASWALI YA MARUDIO:

1) Ni kwa siku ngapi Yesu alionekana kwa wanafunzi wake baada ya kufufuka kwake?.

(2) Yesu aliahidi nani atakuja baada yake?

(3) Yesu alirudije mbinguni?

(4) Wanafunzi walienda wapi na walifanya nini baada ya Kristo kurudi mbinguni?.

(5) Yuda alifanya nini bada ya kumsaliti Kristo.

(6) Ni nani aliyechaguliwa kujaza nafasi ya Yuda?

Wanafunzi walikuwa bado wamekusanyika kule orofani wakati siku ya Pentekoste ilipotimia. Pentekoste ilikuwa sikuku kubwa ambayo wayahudi. Walisherekea kila mwaka, sherehe ya Malimbuko ya kwanza ya mavuno. Katika siku hii, wakati wanafunzi na wafuasi wa Kristo walipokuwa wamekusanyika pamoja, ahadi ya Kristo ilikuja.

Ghafla walisikia sauti kutoka mbinguni ilikuwa kama sauti ya upepe mkubwa wenye Nguvu. Kilichoonekana upepo Mkubwa wenye nguvu. Kilichoonekana ni kama ndimi za moto zilizomkalia kila mmoja ndani ya nyumba wote wakajazwa na Roho mtakatifu na kuanza kunene kwa lugha kama roho alivyo waongoza.

Wayahudi wacha Mung (watauwa) kutoka kila mahali katika ulimwengu uliokuwa unfahamika walikuwepo katika mji wa Yerusalemu kuhudhuria sikukuu ya Pentekoste. Waliposikia ile sauti kubwa walikuja mahali wanafunzi walipokuwepo watu walichangayikiwa kwa sababu kila mmoja aliweza kuelewa ambacho waumini walichokuwa wakikisema kwa lugha zao wenyewe.

Walishangaa ni jinsi gani wanaume hawa kutoka Galilaa (au kaskazini mwa Isarael) wangeweza kunena kwa lugha za nchi kama Misri,Libya Italia, Mesopotamia na Nchi na miji mingine mingi duniani Pote. Wengi walistaajabu walipowasikia watu hawa wanaume na wanawake wakitoa sifa za ajabu kwa Bwana. Hata hivyo wengine kwa kweli, walionea mashaka kilichokuwa kikiendelea na kudhani ya kuwa wanafunzi walikuwa wamelewa.

Petro na wanafunzi wengine wakasimama na kuanza kuhubiri kwa watu walikuwa wakiwasikiliza. Petro akawaambia ya kuwa wanaume wanaonena kwa Lugha mpya hawajalewa . Akaweka wazi kuwa kila mmoja alikua akiona utimilifu wa ahadi iliyotolewa katika kitabu cha Nabii Joel . Hii ilikuwa ahadi ya Roho Mtakatifu.

Petro akawaeleza mambo mengi juu ya Kristo akasema kwamba umati ule walimsulubisha Kristo siku chache zilizopita yeye asiye na hatia. Kristo alidhihirisha ya kuwa yeye ni nani kwa kufanya miujiza mingi. Hata hivyo Mungu alimfufua katika kaburi kwa sababu mauti haikuwa na mamlaka kwake. Akaeleza juu ya mfalme mkuu mmoja wa wayahudi na nabii, Daudi alivyosema ufufuo wa Kristo. Akasema kwamba sasa Kristo yuko mkono wa kuume wa Mungu, na amemtuma Roho Mtakatifu kwa wote kuona na kusikia. Petro akamalizia kwa kusema kuwa Israeli wote wajue kwamba Yesu ni Bwana na Kristo.

Petro alipomaliza kusema, watu wengi walipata mguso mkubwa wa kiroho , na wakawauliza wanafunzi kuwa walipaswa wafanye nini. Petro akajibu “Tubuni na kubatizwa kwa jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho mtakatifu . Maana ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu”.

Baada ya Petro kuhubiri kwa muda mrefu kidogo watu elfu tatu kwa furaha wakapokea yale aliyoyasema nao wakaongezeka katika Kanisa. Baada ya hapo, waamini wote wapya wakakusanyika pamoja na kuwa na ushirika wakila na kusali pamoja . Na Mitume(wanafunzi) wakafanya miujiza mingi . Kila mmoja aliyemwamini kristo wakakusanyika pamoja na kuwa na vitu vyao vyote shirika. Wakaendelea kuabudu pamoja katika hekalu la kiyahudi na kula pamoja katika nyumba ya kila mmoja wao. Waamini hawa wapya.

Walifanya mambo haya kwa furaha ya kweli na imani rahisi. Walimsifu Mungu na kupata heshima miongoni mwa raia wa nchi yao. Mungu akalikuza kanisa kila siku kadiri watu wengi walivyokuja kumwamini Yesu Kristo.

MASWALI YA KUJADILI:

1. Wayahudi walikuwa wakija Yerusalemu kusherekea sikuu. Jina la sikukuu hiyo ni nini?

2. Kulitokea nini kwa wanafunzi wa Yesu siku ya Pentekoste?

3. Wayahudi kutoka duniani kote walifikiri nini walipo wasikia wanafunzi wakisema kwa lugha zao?.

4. Ni nani aliyesema na watu wote waliokuwa wamekusanyika?.

5. Watu wangapi waliyatoa maisha yao kwa Yesu baada ya hotuba ya Petro?.

6. Eleza jinsi kanisa la Kwanza lilivyokuwa baada ya waumini hawa wapya kuingia kanisani.

KWELI ZA KIROHO.

1. Enzi mpya yaanza.

Siku ya Pentekoste, Mungu alimtuma roho mtakatifu kwa wafuasi wa Yesu. Alifanya hivi kwa njia ya miujiza mikubwa iliyoonyesha wale waliokuwepo kwamba huduma ya Roho Mtakatifu kwa Kanisa imeanza. Roho mtakatifu amefanya kazi katika umilele wote, lakini huduma yake kwa Kanisa ilianza siku hii. Mungu aliwaonyesha watauwa wa Kiyahudi kutoka duniani kote kwamba siku mpya imewadia.

Mtu ayatoapo maisha yake kwa Kristo, biblia inafundisha kwamba humpokea Roho Mtakatifu (1Wakorintho 12:13) Kama tulivyojifunza katika somo la juma lililopita, roho Mtakatifu ana huduma nyingi kwa waumini wapya, lakini mojawapo ya huduma hizo ni kumpa kila mwamini ndani ya Kanisa KARAMA ZA KIROHO . Karama hizi ni zana ambazo Mungu huzitumia kupitia kwetu kutusaidia kumtukuza na kulijenga Kanisa lake.

Tunaweza kujifunza nyingi za zana hizi katika waraka kwa warumi 12 na 1 Wakorintho 12 pia Roho hutupa karama hizo kama vile kuhubiri, kufundisha, Imani,utoaji na uongozi na zingine nyingi zilizoorodheshwa katika Maandiko. Tangu mwanzoni mwa Kanisa lako jipya, kila mshiriki anapaswa aangalie na kuona karama zake zenye msukumo zaidi ni zipi. Biblia haikupi kikomo cha kutumia karama moja tu. Unaweza kugundua kwamba kuna karama kadhaa ni zaidi ya nyingine. Unapo baini karama yako, chunguza kuona eneo unapojisikia vizuri zaidi na furaha kubwa zaidi sana katika kulisaidia Kanisa. Inawezekana zoezi hili likawa la kujaribia na kukosa, lakini

nojawapo ya kanuni za Kanisa lenye afya ni kwamba waumini wote wawe watendaji hai katika mwili wa Kristo.

Karama moja ambayo imekuwa ngumu sana kwa makanisa mengi kuielewa ni karama ya ndimi au kunena kwa lugha. Katika siku ile ya Pentekoste, waumini wote wa Mungu, kwa muujiza kabisa walipewa uwezo wa kuzungumza kwa lugha toka dunia nzima.

Siku hii ya Pentekoste kidogo kuna utofauti na kile ambacho makanisa ya kububujika kwa kunena kwa ndimi / kwa lugha.

Tunasoma kutoka katika maandiko kwamba hakuna karama hata moja ambayo imetolewa kwa waumini wote muda wote (1kor. 12:4-11). Katika tukio hili tunaona Bwana wetu anawapa uwezo wa kuzungumza kwa lugha nyingine waumini wote. Hii ilikuwa ishara siku mpya kwa Wayahudi. Kwa ajili ya kujifunza katika hali hii hii ya kuamiminwa kwa Roho kwa Wasamaria (watu waliochanganyikana damu na wayahudi),

Soma Matendo 8.
Pia kwa ajili ya kujifunza juu ya tukio hili / ishara hii ya ilitolewa kwa watu wa mataifa soma (Matendo 10.)

Pia ishara hii ilitolewa kwa Waumini wa Agano la kale, au Wafuasi wa Yohana Mbatizaji, soma (Matendo 19)

Miaka elfu mbili baadaye bado kuna mjadala mkubwa wa Kitheologia kuhusu Karama ya kunena. Baadhi ya makanisa hufundisha kuwa karama hii ilikoma baada ya wakati wa wanafunzi, baadhi ya makanisa hufundisha kuwa karama hii bado inaendelea hata leo.

Bado pia kuna mjadala mkubwa juu ya, Je, lugha zilizosemwa na wanadamu wakati huo huo wengine wanaamini kuwa "**Kunena kwa ndimi au kwa lugha"** ni kwa kutumia lugha ya Kiinjilisti ambayo hatuwezi kuielea bila ya mtafsiri.

Wewe na kanisa lako inawapasa kuendelea kuomba juu ya kile mnaamini maandiko yanafundisha juu ya kuwa makanisa mengine ambayo hata ni mazuri kuliko lako, yanweza yasishikilie mtizamo ambao wewe unao. Hali hii haipaswi kuwa kiini cha mgawanyiko wa Kanisa.

2. **Mara zote kutakuwa na watu wenye mashaka (Matendo 2:13)**
Hata pamoja na yote yaliyotokea siku ya Pentekoste, watu wengi walidhani kuwa wanafunzi walikuwa wamelewa na kile kilichokuwa kikitendeka lazima ilikuwa ni uongo / hila.

Mara zote kanisa lako litakumbana na watu wanaotilia mashaka ya kile mnafanya na wakati mwingine kudhihakiwa hadharani au hata kuteswa. Je, umeshawahi kukutana na wenye kutilia mashaka na kukejeli iamani yako?

3. **Kusudi la pili la tatu la kanisa ni USHIRIKA** na **IBADA (Matendo 2:40 – 47)** tunapolisoma kanisa, tutaangalia makusudi saba ya msingi ya kanisa kila kitu ufanyacho laizma kiwe kimelenga kutimiza moja ya makusudi hayo. Hii italisaidia kanisa kulinda mwelekeo na mtizamo katika majukumu yake ya muhimu .

Kumbuka kuwa Kanisa zuri ni lile lenye uwiano wa makusudi yote **SABA**. Katika somo hili, makusudi haya hayajawekwa katika mlolongo wowote ambao una umuhimu Fulani makusudi yote ni muhimu.

Kusudi la pili ni **USHIRIKA**. Kama biblia inavyolielezea kanisa la kwanza tunaona kwamba kanisa lilifanya mambo kwa "**Moyo wa furaha**" na wakapata heshima kutoka kwa watu wakapata heshima kutoka kwa watu katika Yerusalemu. Tunaona kuwa walikula pamoaja waliabudu pamoja. Pia walishirikiana au walitumia pamoja pesa na vitu mbali mbali walivyokuwa wakimiliki. Walikaa kama familia moja

Biblia inatuambia kuwa mara unapokuwa umeyatoa maisha yako kwa Kristo basi unakuwa umeipata katika familia ya Mungu. Kanisa linaitwa Bibi Harusi wa Kristo (ufunuo 22:17) na anakupenda.

Wewe ni sehemu ya familia ya Mungu ambayo misingi ya maisha yake ni Kristo. Inakupasa kuweka nadhiri ya kukutanika pamoja kuomba na kupata muda wa kukaa katika ushirika wa pamoja. Furaha mnayoshiriki pamoja ni ya kweli. Watu wengine wanapaoona upendo baina yenu wanatamani na wao pia kuona upendo waKristo katika Maisha yao.

Ikiwa sasa wewe tena. Hata kama ni wewe pekee katika familia au ukoo wako uliyeamini, sasa unafamilia katika Kristo ambayo inaweza kukupatia upendo na msaada wowote unaohitaji.

Je, ni jinsi gani mnaweza kufanya ushirika pamoja? Biblia inatupa mifano kadha wa kadha. Tayari tumekwisha kutaja ushirika wa kula chakula pamoja kupumzika pamoja na marafiki ni zaidi ya kupika na kula pamoja. Kukutanika pamoja na kuabudu pia ni njia nzuri ya ushirika.
Ushirika ni kuwa na wakati wa kufurahi pamoja.

Najua kuwa baadhi ya makanisa huwa hayatoki na kwenda kujumuika na wengine kwa pamoja. Ushirika wao umejikita tu katika huduma.

Pamoja na hayo yote, ushirika ni wakati wa kuionyesha ulimwengu furaha na upendo ulio baina yenu kama Wakristo mwaweza kucheza mpira, kufanya sherehe au kitu chochote mnachoweza kufanya pamoja na kufurahi kama familia.

Kama uko katika nchi ambayo hamuwezi kukutana pamoja kwa ajili kufurahi, jaribu kuona namna ambayo mtaweza kufanya ushiriki wenu pamoja. Ni kwa namna gain? Kama haiwekani kukutana pamoja kama kundi kwa jaili ya ushirika, basi mkutane pamoja mmoja mmoja, Wawili au watatu wanaweza kukutana kwa siri kwa ajili ya ushirika ili kuinuana kiimani.

Sasa tumeshajadili ushirika, hebu tuangalie kusudi la **KUABUDU.**
Katika kusoma matendo 2, utaona kuwa ibada ilikuwa na mchango mkubwa katika Kanisa la kwanza na maisha yao ya kila siku. Utawaona washirika wakikutanika pamoja na kumsifu baba kwa kila jambo alilo litenda katika maisha yao. (Matendo 2:47) unaweza kuona sehemu hii ya maombi na kuabudu katika matendo yote.

Baada ya Kristo, kupaa zake mbinguni wanafunzi wake walikusanyika ili kuomba (maendo 1:14). Ingawaje maandiko katika kifungu hiki yanajadili katika sura ya maombi, tunaweza kujifunza toka sehemu zingine ya kuwa pia walijibiisha katika kumsifu Mungu pia.

Kitabu cha Luka kinatuambia kuwa " na walimwabudu yeye, na kurudi Yerusalemu wakikwa wamejaa furaha tele, na waliendelea kumsifu Mungu katika Hekalu.
Amina (Luka 24:52,53) kwanini walikuwa wakimsifu Mungu?
Kioongozi wao Bwana Yesu, ambaye alikufa, na hata kufufuka pekee, lakini hata alipaa kwenda mbinguni. Bila shaka walikuwa na mskumo Fulani wakiimawazo wakati huo. Pengine walikuwa katika uchaji na nguvu ya Mungu. Huenda walikuwa katika furaha iliyozidi 40 hapo awali walifikiri kwamba wote wamepotea, lakini wakajua kwa hakika ya kuwa hawakupotea.

Hamu yao ya asili ilikuwa ni kumsifu na kumwabudu Mungu kwa yale ylaiyokuwa yakitendeka miongoni mwao
Katika mifano yote hii ya ibada ya kweli unaweza pia kuona kipengele ambacho Biblia imekitaja sana nacho ni umoja wa waumini
(Mdo 1:14, 2:1, 4:24)

Kundi lako la waumini linapoanza kufanyia uchunguzi juu ya aina za ibada, kumbuka kuwa ibada ya kweli huja wakati mnapokuwa katika umoja. Ni

vigumu sana kumwabudu Mungu kama unachuki na mtu aliyeketi kando na wewe.
Ibada ni njia ya Mungu kuturuhusu kumpa heshima anayostahili Biblia inatuambia kuwa Mungu anastahili kusifiwa. **KILA JAMBO** tufanyalo yapaswa liwe tendo la kuabudu / kumpa sifa Mungu wetu.

Kutoa, Kuhubiri, Kufundisha, Kujifunza, Kufanya Uinjilisti yote yapaswa yawe na mwelekeo wa kuabudu.
Ingawaje kuabudu kunaweza kuwa kwa mtu mmoja mmoja, ni muhimu pia kuwe na ibada ya ushirika

Je, unaweza kuanza ibada ya ushirika? Inawezekana tayari umekwisha kuanza kuabudu kama kundi. Kama umekuwa ukikifuatilia kitabu cha Uinjilisti wa kiuvumbuzi ulikuwa tayari umeulizwa, kuweka sura za ibada, kama vile kuimba, na katika kujifunza.

Tunaweza kupendekeza kuwa hakuna muda mzuri wa kuanza ibada kama kundi ulio mzuri kama sasa.
Usitupilie mbali kuabudu kama kundi, anza mapema iwekanavyo.

Somo hili halikuandaliwa ili kukupa hatua kwa hatua juu ya namna ya kuendesha ibada, lakini tunapendekeza kuwa uweka, maombi, sifa kupitia uimbaji, ushuhuda matoleo, kufuata sheria au maagizo na labada kipindi cha maswali na majibu, kama sehemu ya ibada.
Mara kwa mara huwa tunafikiri kuimba pekee ndiyo ibada, lakini yote yaliyotajwa hapo juu ni matendo ya ibada.

Pia kuna njia nyingi unazoweza kumwabudu Mungu. Buni ibada yako katika hali halisi ya mzingira ili kuwapa watu fursa ya mzingira ili kuwapa watu fursa ya kumsifu baba.

Huko Brazil waumini hupenda kuimba, kuimba na kuimba. Huko Amerika waumini wanaonekana kuwa wanapenda kuimba kidogo na kisha mahubiri mengi.
Hapa Afrika, waumini hupenda kucheza katika kumtukuza Bwana
Weka pamoja hayo yote, au na mawazo mengine kwa kadri unavyoona inafa.
Weka muda wa kutosha kwa ajili ya ibada ili watu wako waweze kufurahia.

Weka mtiriko wa matukio katika ibada ili watu wafurahie. Inakupa ufanye maamuzi kile kinachofaa zaidi katika utamaduni wako.
Kumbuka kuabudu kwa pamoja na kwa utaratibu, ukiiruhusu biblia iwe mwongozo kamili wa kila jambo ufanyalo.

Katika somo lifuatalo, tutakwenda kuona jinsi kanisa lilivyoendlea kukua kupitia kazi za watu wa kawaida kabisa waliokuwa wakitafuta kuhudumu kwa ajili ya Bwana Yesu.

SOMO LA 3
Huduma ya kanisa hapanuka
(Huduma)

Matendo 3 na 4

Kifungu cha msingi: “sina fedha wala dhahabu,lakini nilicho nacho ndicho nikupacho.Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti simama uende.”

Maswali :-

1. Ni nani aliyeahidiwa na Yesu Kristo kuja badala yake?
2. Kilitokea nini siku ya Pentekoste.?
3. Je,kila mmoja aliamini kile kilichokuwa kikitokea siku ya Pentekoste?
4. Ni watu wangapi walimwamini Yesu baada ya Mahubiri ya Petro?
5. Elezea baadhi ya mambo ambayo kanisa lilifanya baada ya kuyatoa maisha yao kwa Kristo.

Petro na Yohana wakaenda Hekaluni kusali yapata saa tisa za mchana.Kulikuwa na mtu mmoja kiwete aliyeketi katika malango ya kuingia Hekaluni kila siku.Akawaona Petro na Yohana naye akawaomba wamchangia.Petro na Yohana wakamuamuru awatizame kisha wakasema, “sina Fedha wala Dhahabu ,lakini nilicho nacho ndicho nikupacho:Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti inuka na utembee.” Wakamsaidia yule mtu kusimama na mara nguvu zikamjia katika miguu na vifundo vya miguu yake.Aliyekuwa kiwete akaruka na kutembea akimsifu Bwana. Watu wote kaika eneo lile wakastaajabu kumuona yule kiwete ambaye walizoea kumwona akiketi malangoni ameponywa na sasa anatembea .

Watu wote wakawaendea ,Petro na Yohana kasha nao wakanza kusema na makutano.Petro akawaambia msitufuate mimi na Yohana.Aliyemponya mtu huyu ni Yesu Kristo.Mtu huyu ameponywa kwa sababu alikuwa na imani katika Jina la Yesu.Petro akawaambia makutano ya kuwa walimsurubisha Yesu kwa sababu ya ujinga,lakini sasa ni wakati wa kutubu dhambi zao.Akasema, “tubuni muokolewe,ili dhambi zenu zipate kuondolewa,ili mpate wakati wa kufurahi katika uwepo wa Bwana.”

Petro na Yohana walipokuwa wakisema,makuhani na viongozi wa dini wakawaendea.

Walikasirika sana juu ya Petro kuhubiri habari za kufufuka kwa Kristo.Wakawakamata Petro na Yohana na kuwafunga Gerezani.Hata hivyo,watu wengi waliamini na siku hiyo idadi ya watu katika kanisa ikaongezeka na kufikia elfu tano.

Petro na Yohana wakapelekwa kwa wakuu wa dini ili wakahukumiwe.Wale wakuu wa dini wakawauliza, je, ni kwa mamlaka gani au kwa jina la nani walikuwa wakitenda miujiza yao.Petro akajibu, “ akasema tumemsaidia yule Kiwete kutembea kwa nguvu na mamlaka ya Yesu Kristo.Petro akawaambia ya kuwa, “ hakuna wokovu kwa namna nyingine yoyote,kwa kuwa hakuna jina jingine chini ya mbingu,lililotolewa kati ya mwanadamu ambalo yatupasa kuokolewa kwalo.”

Wale viongozi wa dini waliweza kuona kuwa Petro na Yohana walikuwa watu wa kawaida tu,wasio na elimu lakini walishangazwa na kile walichokuwa wakisema.Wale

wakuu wa dini wakakutana kwa faragha kwa pamoja nakufanya maamuzi kuwa hawawezi kuukana muujiza ulitendeka,lakini wakaamua kuwaamuru Petro na Yohana wasiendelee tena kuwaambia watu wengine juu ya habari za Yesu.Petro na Yohana wakajibu na kusema, " wao watamtii Mungu na wale si amri ya mwanadamu.Wale makuhani wakawatisha Petro na Yohana,lakini hawakuweza kuwaadhibu kwa sababu ya umati mkubwa wa watu uliokuwa ukimtukuza Bwana kwa yale yaliyokuwa yametendeka.kila mtu akaanza kumtukuza Mungu kwa kile alichofanya.Kanisa likamwomba Mungu alipe ujasiri wa kuihubiri injili,na ili miujiza na uponyaji zaidi viendelee kutendeka zaidi na zaidi.Biblia inasema walijazwa na Roho mtakatifu na wakahubiri neno la Mungu kwa ujasiri.

Maswali:-

1. Ni wanafunzi wapi wawili walioenda Hekaluni kusali?
2. Yule kiwete alikuwa anahitaji nini, na nini alichopokea badala yake?
3. Je wale wakuu wa dini walifurahiswa na kile kilichotokea?
4. Je, Petro na Yohana waliamuriwa kufanya nini na wakuu wa dini? Je, Petro na Yohana walichagua kumtii nani?
5. Petro na Yohana walienda wapi mara baada ya kuachiliwa huru?
6. Je,kila mtu alifanya nini baada ya Petro na Yohana kurudi,na maombi yao waliyaelekeza kwa nani?

Kweli za Kiroho:

1. Sina Fedha wala Dhahabu……(Mdo 3:6)

Watu wengi duniani wangependa kuwa na pesa nyingi.Vivyo hivyo makanisa mengi yangependa kuwa na pesa nyingi ili yaweze kufanya huduma nyingi zaidi. Pamoja na hayo tunaona ya kuwa toka mwanzo wa kanisa tunakuta kuwa waumini wengi,hata viongozi,hawakuwa watu matajiri.Petro na Yohana walikuwa miongoni wa viongozi wa msingi katika kanisa la kwanza,lakini siku ile walikuwa wakitembea bila hata pesa.

Makanisa mengi katika historia yote ya ukristo hayajakuwa na utajiri mwingi.Pengine kanisa lako si tajiri lakini Mungu anataka kukutumieni katika njia ambayo si ya kawaida.Atakutumia wewe sawasawa tu na alivyowatumia wakristo wengine katika ulimwengu huu yapata karibu miaka 2000.Usione aibu na kufungwa na pesa.Mungu atatumia alichokupatia katika kukuza ufalme wake.

Kwa namna nyingine, kama Mungu amekubariki kuwa na pesa,mshukuru kwa ajili ya baraka hiyo.Pamoja na hayo,Petro na Yohana walijua kuwa hitaji la kweli kwa yule kiwete halikuwa kuponywa pekee,lakini ni kuwa na imani katika Bwana.(Mdo 3:16)Tumia fedha yako kwa hekima kwa ajili ya ufalme ili kuwasaidia wengine wawe na "imani kwa jina Lake".

2. **Petro na Yohana walikuwa wakienda kusali lakini walisimama ili kutoa msaada,KUHUDUMIA mtu aliyekuwa akitaabika.(Mdo 3:4)**

Kusudi la nne la kanisa ni HUDUMA.Kwa lugha nyingine ni kwamba,kanisa linapaswa kwenda na kuwatafuta watu na si kuwahudumia kiroho,lakini pia katika mahitaji ya mwili na kiakili.Petro na Yohana walikuwa wakielekea Hekaluni kusali.Tumekwisha kujifunza kuwa maombi yanapaswa kuwa msingi wa kila jambo ambalo tunataka kufanya ili kupata uongozi wa Roho mtakatifu katika kila jambo. Hawa wanafunzi wawili walikuwa wakifanyua kilekile walichopaswa kufanya wakati huo. Petro na Yohana waliweza kusimama ingawa walikuwa wakienda kufanya kazi ya msingi sana(kuomba),hapa Bwana aliwaongoza kufanya kitu kingine tofauti kabisa. Mungu aliwataka wamsaidie yule mtu kimwili na Kiroho.
Mungu ameliunda kanisa ili liwe kama muundo mbinu wa kuusaidia ulimwengu unaotaabika. Si jukumu la serikali pekee kuwasaidia wahitaji.Ni jukumu letu kama kanisa kuwasaidia wanaotuzunguka. Kwa nini tunapaswa kufanya hivyo? Je ,uliona kilichotokea baada ya yule mtu kuponywa? **Alimsifu Mungu.** Watu wote waliokuwa karibu na yule mtu waliona yakitokea. Hivyo unapowafikia wengine katika jina la Yesu,ulimwengu utaona upendo wa Kristo kupitia wewe na atapata utukufu kwa sababu ya matendo yako ya utii.
Ni jinsi gani kanisa lako laweza kuufikia Ulimwengu unaohangaika ili kukutana na mahitaji yake ya kimwili na masikitiko yake?
Je,waweza kununua chakula kwa ajili ya familia yenye njaa?
Je, waweza kuwafunza watu wazima namna ya kusoma ili waweze kujitafutia Ajira?
Je unaweza kuwa rafiki wa familia waliopata mtoto hivi karibuni ili kuwasaidia awweze kulea mtoto wao?
Je, unaweza kuwatembelea walio wagonjwa au wazee?
Sisi kama kanisa tunahitaji kusimama na kuomba Mungu atuonyeshe namna ambayo tunaweza kuuhudumia ulimwengu utabikao.
Kanisa sit u kwa ajili ya kuuhudumia ulimwengu, yawapasa pia kuwahudumia hata walio **ndani ya kundi** kama kanisa wenye mahitaji.Kama tulivyoona katika sura iliyopita,kanisa lilikuwa linakutana na mahitaji ya ndugu na dada katika Kristo.(Mdo 2:45) Je, kuna yeyote katika kundi lako ambaye anaweza kuwa na hitaji,kimwili,kifedha au amesongwa na mawazo sasa hivi? Omba ili Bwana akuonyeshe namna ambavyo waweza kusaidia mahitaji kama hayo.
Kusudi hili la HUDUMA ni kwa ajili ya kanisa zima.Biblia inatuonyesha wazi kuwa Mungu ameweka karama ya HUDUMA.(Rum 12:7) Kila muumini yampasa kushiriki katika kusudi la huduma. Usisahau kuwa,tumeona ya kwamba wakati mzuri wa kuanza kuhudumia wengine ni MWANZO wa kanisa,msingojee hadi kanisa litakapokuwa kubwa au kukomaa. Ukiijenga tabia hiyo mapema, itabaki ndani yenu wakati wote wa huduma ya kanisa, na Mungu ataibariki.

3. Viongozi wa dini walikuwa wanajua ya kuwa Petro na Yohana si wasomi(Mdo 4:13)

Mungu hutumia watu wa kawaida kabisa walio na unyenyekevu wa kutosha ili kulikuza kanisa lake.Petro na Yohana walikuwa watu wa kawaida kabisa wavuvi wa samaki ambao Yesu aliwachagua.Watu hawa walimruhusu Roho mtakatifu wa Bwana kuwaongoza katika kazi zao.Pia walifanya mambo ya miujiza mikubwa,na kuhubiri mahubiri yenye ujumbe mkuu, na waliwaona watu maelfu kwa maelfu wakija kwa Bwana. Pia usisahau kuwa Petro na Yohana walijua kuwa mambo hayo yote yalikuwa wakitendeka si kwa nguvu zao,lakini kwa nguvu za Kristo aliyewatuma.Watu walipotaka kuwaabudu waliwahakikishia kuwa si wao wafanyao hayo yote bali ni kwa nguvu ya Bwana.(Mdo 3:12)

Mungu anataka kukutumia wewe pia.Wengi wetu ni watu wa kawaida tu.Wala si maarufu.Wala hatuna nguvu,lakini tunataka kuwa watum,ishi wa Mungu.Kusema kweli,Mungu anatuambia kwa makusudi mazima huchagua watu wa kawaida katika dunia hii ili kukamilisha makusudi yake.(soma 1 kor 1:26-31)

Katika somo lifuatalo tutaona jinsi dhambi ilivyoanza kulinyemelea kanisa na jinsi Bwana alivyoshughulika na suala hili.

SOMO LA 4
Kanisa linashambuliwa kutoka ndani
(Ufuasi)
Matendo 4 na 5.

Kifungu cha msingi:Petro akasema,Anania kwa nini shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho mtakatifu,na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja?" Matendo 5:3

Maswali ya mdomo:

1 Kilitokea nini katika siku ya Pentekoste?
2 Je,makutano walifanya nini baada ya mahubiri ya Petro?
3 Je, Biblia inasema kanisa la kwanza walifanya nini kwa pamoja baada ya watu wengi kuokoka?
4 Ni wanafunzi wapi wawili walioenda kuomba Hekaluni?
5 Ni nani waliyemponya na kitu gain kilitendeka?
6 Je, viongozi wa dini walichukua hatua gani?
7 Petro na Yohana walisema nini?

Kanisa lilikuwa katika umoja kamili.Kila mmoja aliyekuwa sehemu ya kanisa walishiriki kila kitu walichokuwa nacho.Wengi waliomiliki majumba na mashamba wangeliuza na kutoa walichopata kwa mitume na kwa kanisa.Kwa mfano,mtu mmoja aliyeitwa Barnaba(jina lenye maana ya mwana wa kutia moyo) aliuza shamba lake na kutoa kanisani.
Pia, kulikuwa na mke na mke kwa majina Anania na Safira.Nao waliuza shamba lao na kutoa kwa mitume,lakini hawakuwa waaminifu wa kusema wazi thamani halisi ya shamba.Anania aliwaambia viongozi wa kanisa kwamba atatoa sehemu yote ya kile kitakachopatikana kwa ajili ya kanisa,badala yake,wakaficha sehemu ya pesa zilizopatikana kwa ajili ya matumizi yao binafsi.Petro akampinga Anania. Akamuuliza kwa nini umemdanganya Roho mtakatifu na kuficha sehemu ya pesa.Baada ya kusikia maneno haya toka kwa Petro,Anania akafa.

Masaa matatu baadaye Safira mkewe, naye akawasili.Petro akamuuliza thamani ya shamba ilikuwa kiasi gani? Naye pia akasema uongo juu ya pesa walizopata.Petro akamwambia nawe pia utakufa kama mmeo maana umesema uongo.Ghafla akaanguka miguuni mwa Petro na akafa.Kisha kanisa wakamzika na hofu kuu ikalikumba kanisa..

Mitume waliendelea kufanya "ishara na maajabu mengi miongoni mwa watu", na kanisa likaendelea kukua.Watu wengi walienda ili kuponywa na mitume pamoja na Petro.Makutano walijaribu hata kupata kivuli cha Petro kwa matumaini kuwa watapokea uponyaji.Watu wa Yerusalemu wakalipa kanisa heshima kubwa.

Siku moja kuhani mkuu wakawakamata makuhani na kuwafunga Gerezani,lakini usiku ule Malaika wa Bwana akawafungulia na kuwaambia warudi hekaluni kuhubiri. Asubuhi iliyofuata makuhani walitaka wakaletwe hao mitume toka kule Gerezani kwa ajili ya kuhojiwa,lakini wale askari waliotumwa kwenda kuwachukua, waligundua kuwa wamekwisha toweka hawamo tena Gerezani.Wakasikia kuwa wako Hekaluni wanahubiri.Wale askari wakaenda kwa utulivu na kuwaleta wale mitume(waliogopa kwenda kuwachukua kwa nguvu kwa sababu ya watu waliokuwa wamewazunguka) Wakawauliza wale mitume kwa nini wanaendelea kuhubiri kuhusu Kristo wakati walikuwa wamekwisha kuambiwa wasifanye hivyo.Wale askari wakawaambia mitume ya kuwa “mmeijaza Yerusalemu yote na mafundisho yenu.” Petro na wale mitume wengine wakawaambia askari kuwa, “yatupasa kumtii Mungu.”Inawapasa kuhubiri kuhusu Yesu Kristo ili watu watubu Dhambi.

Wale viongozi wa dini wakakasirika sana na wakataka kuwaua.Mtu mmoja miongoni mwa viongozi wale wa dini,aliyeitwa Gamalieli,akawasihi wasifanye hivyo.Akawakumbusha juu ya watu hapo nyuma waliojaribu kuibadili Israeli lakini waliambulia patupu.
Akawaambia kuwa “kama haya mafundisho yatoka kwa Mungu,hamuwezi kuyazuia,la sivyo mtajikuta mnapigana na Mungu.”

Wale viongozi wakakubaliana na Gamalieli.Wakawaachia wale mitume bila hata kuwapiga.Wakaonywa tena kutohubiri jina la Kristo Yesu.Kisha mitume wakaondoka zao kwa furaha kwa kuwa wameweza kuteswa kwa sababu ya jina la Yesu.Waliporudi kila siku siku walifundisha na kuhubiri katika mahekalu,na katika miji ya watu juu ya Yesu Kristo.

Maswali:

1 Anania na Safira ni nani?
2 Kitu gani kiliwatokea baada ya kusema uongo mbele ya mitume?
3 Kwa nini watu wengi walikwenda kuwaona Mitume?
4 Viongozi wa dini waliwafanya nini Mitume?
5 Je,Mitume walitokaje Gerezani?
6 Je,kiongozi wa dini Gamalieli alisema nini juu ya kanisa?
7 Je,wale mitume walifanya nini baada ya kufunguliwa toka Gerezani?

Kweli za kiroho:

1 Watu wa kanisa walipeana(Mdo 4:32-37)

Mwanzo wa kanisa la kwanza,ni wazi kwamba watu walikuwa na upendo mkuu.Walionyesha upendo huo kwa kutoa.Hata walianza kuuza walivyo navyo ili waweze kuwasaidia waliokuwa na mahitaji.
Mungu hahitaji pesa zetu.Yeye tayari anamiliki kila kitu.Yeye hutumia pesa tunazotoa kwa ajili ya kutimiza makusudi yake.Kanisa lako linapoanza unahitaji kuanza kwa

kuwahudumia wenye mahitaji maalumu walio kanisani na walio nje ya kanisa. Usiogope kusema juu ya mahitaji,kutoa moja ya kumi na sadaka ili kanisa lako liweze kutenda kazi. Kutoa fungu la kumi(au 10% ya mapato yako) na sadaka na zaidi ya 10% ni matendo ya ibada au kwa lugha nyingine ni sehemu ya kumwabudu Mungu.Zawadi kama hizi zaonyesha heshima kwa Bwana na kuonyesha ya kuwa vyote unavyomiliki ni vya Bwana.

Kanuni ya kutoa fungu la kumi ni ya tangu nyuma katika mwanzo wa historia ya kibiblia, nyakati za Agano la kale(Malaki 3:6-12),Waebrania 7:2 .
Kwa ujumla,siku ya Pentekoste,au siku ambayo Roho mtakatifu alianza huduma yake katika kanisa,ilikuwa wakati wa sherehe ya malimbuko ya kwanza(matunda ya kwanza). Huo ulikuwa wakati ambapo Waisraeli walishiriki baraka zao za awali kutoka katika mavuno ya mazao yao.Mungu alichagua kuanzisha kanisa wakati huu ambapo Wayahudi walisherehekea sherehe ya utoaji wa dhabihu.

Mchungaji wako au kiongozi hapaswi kuona aibu kusema na washiriki wake juu ya utoaji wa pesa kanisani.Kanisa zima lapaswa kupata heshima kwa kutoa fungu la kumi kwa ajili ya Bwana kanisani.Je umewahi kuzungumza na washiriki wenzaji juu ya fungu la kumi na sadaka? Je mmekwisha kuamua kuwa ni nani au kundi gani watasimamia hizo fedha? Kumbuka kuna watu ambao wamepewa karama ya usimamizi.Ombeni ili Bwana awaonyeshe ni nani atakayesimamia fedha na kitu gani kanisa litafanya na hizo fedha za fungu la kumi na sadaka.

Jambo jingine la muhimu sana,kumbuka maandiko yanatufundisha kuwa kiongozi wako wa kanisa anahitaji kulipwa(1Kor.9). Kama kiongozi/mchungaji anafanyakazi ya kuongoza,kufundisha na kuwakinga ninyi, hivyo ni wajibu wenu kuhakikisha kuwa yeye na familia yake wanatunzwa pia. Je mmewahi kuzungumza juu ya kumtunza mchungaji wenu kifedha?Je mmewahi kuwaza juu ya gharama ambazo huenda amepata kwa sababu ya kuliongoza kanisa?Je mmewahi kujiuliza ni masaa mangapi hutumia kuongoza,kusoma neno na, kushuhudia ili kuliongoza na kulielekeza kanisa? Labda humuwezi kumsaidia kiongozi wanu katika huduma wakati wote.Na labda inamlazimu kupata kibarua cha muda ili aweze kupata mahitaji.Hii pia ni Kibiblia.Baada ya yote, mtume Paul alikuwa na kazi mbili(Mdo 18:3). Alikuwa fundi wa kutengeneza mahema na hapo hapo mmishenari! Pamoja na hayo, wewe na kanisa lako yawapasa kufanya maamuzi baada ya kuomba juu ya namna kumtunza mchungaji wenu kifedha.
Hata kama mnaweza kumlipa kiongozi wenu kiasi Fulani kwa mara moja, kwa ujumla kumlipa kiongozi wenu ni ishara ya heshima kubwa na utii.

2 Ukweli na uaminifu katika kanisa(Mdo5:1-12).

Ukweli ulipewa umuhimu wa pekee sana na Bwana katika kanisa lake la kwanza na ndiyo maana aliwaua Anania na Safira kwa kusema uongo juu ya thamani halisi ya shamba walilokusudia kutoa kwa Bwana/kwa kanisa.
Tukumbuke kuwa hayakuwa mauzo ndiyo yaliyowaweka matatizoni.Ni kwamba walipunguza uaminifu wao na kusema uongo juu ya kiasi halisi walichopata kutokana na mauzo ya shamba. Mungu huwa hawaui mara kwa mara waumini wanaposema uongo,la sivyo huenda sisi sote tungelikuwa tulikwisha uawa zamani sana!

Vifo hivyo vilitokea ili kuwaonyesha waumini wakati ule,vivyo hivyo waumini wa leo,ya kuwa kanisa la paswa kuwa na watu walio waaminifu wao kwa wao na mbele za Mungu. Labda Mungu anakwenda kuchukua kundi lenu dogo na kulifanya kuwa kanisa kubwa.Labda kanisa lako litakuwa na kuzaliana na kuwa makanisa mengi.Ingawaje matokeo haya yatakuwa maajabu,hakuna hata jambo moja kati ya hayo ni muhimu kama uaminifu.Ulimwengu unakutizama na unaweza kuuhudumia ulimwengu zaidi kwa vile ULIVYO kuliko kile UNACHOFANYA.

3 Je,ishara na maajabu bado vipo hata leo?(Matendo 5:12)

Mara kwa mara tunaona katika kitabu cha matedno mitume walikuwa wakifanya ishara na maajabu.Mungu alichagua kufanya ishara na maajabu kwa kuwatumia wao.

Mungu ananguvu MARA ZOTE za kuponya na MARA ZOTE kufanya miujiza.Pamoja na hayo hajachagua kufanya miujiza katika kila hali na kila mahali katika historia. Tunapoyaangalia maandiko,tunajifunza kwamba kimsingi Mungu alifanya miujiza yake kwa vipindi vichache tu.Katika agano la kale ilikuwa wakati wa Musa na wakati wa Eliya. Katika agano jipya ilikuwa ni wakati wa maisha ya Yesu na mapema ya hapo,na wakati wa kanisa la kwanza.Mungu alitumia miujiza wakati maalumu na katika hali maalumu ili kijidhihirisha.

Inaonyesha kuwa Mungu hapo mwanzo alitumia miujiza kupitia kwa Kristo na viongozi wa kanisa ili kulianzisha na kuliimarisha kanisa. Alitutumia Roho mtakatifu, ambaye hutuonyesha misingi ya kila siku ya kile Mungu hufanya katika maisha yetu hapa ulimwenguni. Wakati Mungu anapochagua kufanya Miujiza leo hii ni juu yake mwenyewe kufanya maamuzi. Inapotokea,tunafurahi kwa kuwa tunapata nafasi ya kuiona miujiza,lakini hatuwezi kujenga imani yetu katika miujiza pekee.Imani yetu imejengwa katika Kristo.
Ukichukua wakati kupiga taswira kama kikundi mtaanza kukumbuka baadhi ya miujiza ambayo imetendeka katika maisha yenu ninyi wenyewe.Kumbuka wakati Mungu alipofanya tendo la kukulinda au la upendo kwako bila wewe kutambua.Utashangaa ni mara ngapi Mungu hujidhihirisha katika maisha yetu.Mshukuru Mungu kwa nyakati ambazo alitenda jambo katika maisha yako.

4 Ufuasi ni kusudi la tatu la kanisa.(Mdo 5:42)

Katika mfululizo wa masomo haya tayari tumekwisha yaangalia makusudi mengine mawili ya kanisa- Ushirika na huduma.Katika somo hili tunaona kuwa kanisa la kwanza lilitoa umuhimu wa kipekee juu ya UFUASI.
Tunaona kuwa kila siku walikutana katika Hekalu na katika miji yao kwa ajili ya kujifunza kuhusu Kristo.(Mdo 5:42) wakati huo waumini hawakuwa na Agano jipya kama tulilonalo leo hii,lakini walikuwa na Agano la kale pamoja na mashahidi wa wanafunzi/wafuasi.Lakini Mungu ametupa mimi na wewe Biblia iliyo kamili yaani Agano la kale na Agano jipya. Kama mwanini wa Yesu Kristo in muhimu sana kukusanyika na kujifunza ili kumjua Mungu kupitia neno lake.Agano jipya na Agano la

kale yote ni ya muhimu sana katika kumfahamu Mungu na kile anchotaka kutenda katika maisha yako.
Tumekwisha kujifunza ya kuwa maombi yanapaswa kuwa mbele ya kila kitu tunachofanya katika huduma.Vivyo hivyo Biblia ni mwongozo wetu ili kumjua Mungu na mapenzi yake.Bwna anaweza kuchagua kujidhihirisha katika kanisa lako kwa njia nyingi sana,anaweza kudhirisha mapenzi yake kwa kupitia ndoto,kupitia ushuhuda wa waumini wengine,au kupitia mambo ya asili.
Pamoja na hayo,Yeye hujidhihirisha DHAHRI kuwa yeye ni nani na mapenzi yake katika maisha yako kupitia maandiko matakatifu.Biblia ndiyo inapaswa kuwa mwongozo wako wa kumfahamu Baba na mwongozo wa kanisa katika kufuata mapenzi ya Mungu baba. Mungu ametupa maandiko ili tupate nafasi ya kujifunza kuhusu Yeye. Katika 2Timotheo 3:16 tunajifunza kuwa, “Kila andiko,lenye pumzi ya Mungu,lafaa kwa mafundisho,na kwa kuwaonya watu makosa yao,na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadabisha katika haki,”Biblia ina makusudi makuu manne.

Maandiko ni kwa ajili ya :-

1. Kutufundisha kuhusu Mungu.
2. Kutukemea tunapokuwa tumefanya makosa.
3. Kutukosoa na kutelekeza katika unyoofu.
4. Kutuonyesha Jinsi ya kuishi kimungu na maisha ya haki.

Kanisa lako lapaswa kutoa kipaumbele cha kipekee kabisa katika kujifunza neno la Mungu.Kiongozi wako pia anahitaji kujifunza neno la Mungu.Somo la mwisho katika mfululizo wa masomo haya utakufunza namna ya kupata ukweli wa Kiroho kutoka katika Neno la Mungu.Itakuwa ni sehemu muhimu sana kwamba kila mmoja atajifunza namna ya kusoma Neno la Mungu na kupata kuwa na macho ya Kiroho.Kwa kiongozi, mazoezi ni ya muhimu sana kwa kadri anavyowaongoza juma baada juma.

Kila mshiriki wa kanisa anamajukumu ya kufanya katika sehemu ya ufuasi/uanafunzi.Kabla ya yote,unahitaji kuanza KUJIFUASA MWENYEWE kwa kuweka moyoni mwako neno la Mungu.(Zab 119:11). Pendekezo langu ni kwanza tenga dakika 15 za kujifunza neno la Mungu kila siku nyumbani kwako.Inategemea na siku unaweza kuchukua muda mwingi zaidi ya dakika 15, kwa ujumla dakika 15 ni mwanzo mzuri kwa waumini wapya wanapojaribu kujifunza neno la Mungu. Kama unataka kujifunza zaidi juu ya wakati wa faragha na Bwana,soma mfululizo wa pili wa masomo ya Biblia ya Uinjilisti wa Ki-uvumbuzi, “Mwanzo wa maisha mapya katika Kristo.” Kama hauna masomo hayo, unaweza kutumia somo la tisa katika mfululizo katika kitabu hiki kwa ajili ya kujifunza jinsi ya kupata macho ya Kiroho katika neno la Mungu.

Jukumu la pili katika sehemu hii ya ufuasi ni **KUWAFUASA WENGINE.Mchungaji** au kiongozi wako ni lazima awe akijaribu kuwafuasa siku zote,lakini wakati huohuo,kadri mnavyokuwa katika imani,inawapasa kuwa mkiwafuasa wengine.Kwa nini? Kwa kadri kanisa lako linapoendelea kukua, mchungaji/kiongozi ataanza kuwa na majumu mengi hivyo hawezi kuwa na muda wa kutosha kukaa na kila mmoja kwa muda wa kutosha ili kumfuasa.Ni jukumu la kanisa kumsaidia mchungaji katika kuwasaidia waumini wapya kukua katika imani kwa njia ya kuwafuasa au kuwafundisha neno.

Ni pale tu,wewe kama kanisa, utakapoweza kujitoa kwa ajili ya kufuasa wengine,kanisa lako litaanza kujizidisha(2Timotheo 2:2) Kuna watu katika kila kanisa ambao Mungu amewapa karama ya huduma hii ya ufuasi.Ombeni Mungu ili awaonyeshe hasa ni nani apaswaye kuwa katika huduma hii muhimu.
Watu wengine hufikiri kuwa ufuasi ni kufundisha tu.Hii si kweli.Kumbuka,ufuasi si kujifunza neno la Mungu pekee.Kwa ujumla ni kuwa na WAKATI wa kukaa na waumini wapya ukiwafundisha na kuwaruhusu kukutazama wewe.Kristo alichukua miaka akila,kukaa pamoja,kufanya kazi na kucheka pamoja na wanafunzi wake.Wakati huo huo alikuwa akiwafundisha ukweli.Mungu anaweza kukutumia wewe kwa namna hiyo hiyo katika maisha ya kuwafuasa waumini wapya. Waumini wapya wanahitaji kuwa na mtu ambaye wataweza kuomba pamoja naye,kusoma Biblia na kuhudumu pamoja naye.
Katika somo lifuatalo,tutakwenda kuona jinsi mateso kwa kanisa yalivyoongezeka na jinsi kanisa la kwanza lilivyokabiliana na matatizo hayo.

SOMO LA 5

Kanisa linashambuliwa kutoka nje.
(Kugawa Madaraka, Mateso)

Matendo ya Mitume Sura ya 6 na 7
Mstari Mkuu. “Bwana usiwahesabie dhambi hii” Matendo ya Mitume 7:60

Maswali ya ufahamu

1. Kilitokea nini siku ya Pentekoste?
2. Petro alifanya nini baada ya makutano kumwuliza juu ya kilichotokea? Nini ilikuwa mwitikio wa watu baada ya Petro kuwa ameongea?
3. Nani alienda hekaluni kuomba? Kilitokea nini pale?
4. Mwitikio wa viongozi wa Wayahudi ulikuwaje?
5. Kanisa liliwezaje kupata mahitaji yake ya kifedha mwanzoni?
6. Kilitokea nini muda mfupi baada ya kanisa kuanza kushirikishana mambo yote? Anania na Safira ni akina nani?
7. Kanisa linafanya nini kila siku hekaluni na kutoka nyumba kwa nyumba?

Wakati kanisa likikua yalianza malalamiko miongoni mwa waumini. Baadhi ya “Hellenists” au watu wa Kiyahudi walioishi nje ya Israeli hawakujisikia kama wajane wao walikuwa wakipata mahitaji yao ya kila siku ya mchango wa chakula wa kanisa. Tatizo hili lililetwa kwa wanafunzi. Wanafunzi wakaazimia kuwa wangewachagua watu saba wenye hekima na heshima kukabiliana na hitaji hili. Mitume wakasema walichagua watu saba kwa kazi hii ili “sisi tuishike kazi yetu ya kuomba na kulitumikia neno”. Mmoja wa watu hao saba aliitwa Stefano. Aliitwa mtu “aliyejaa imani na Roho Mtakatifu”.

Kisha neno la Mungu likaenea na idadi ya wanafunzi ikaongezeka. Hata viongozi wengi wa dini wakawa wanakuja kwa imani katika Kristo. Stefano alifanya miujiza mikubwa na maajabu katika huduma yake.
Wayahudi wengi kutoka nje ya Yerusalemu wakaanza kumjadili Stefano, lakini hawakuweza kumshinda. Wakafanya shauri dhidi yake ili kusema kwamba amesema mambo kumdhihaki Musa na Mungu na wakampeleka mbele ya baraza. Walipokuwa wakimshtaki kwa kile walichokidai kuvunja sheria zao, watu wa lile baraza waligundua kuwa uso wa Stefano ulibadilika na kuonekana kama uso wa malaika.

Kisha Stefano akaulizwa kama hayo mashtaka yalikuwa ya kweli. Katika jibu lake akatoa historia kwa ufupi juu ya Israeli. Hapa akaongea kuhusu jinsi baba wa Waisraeli, Abrahamu alivyoitwa kuiacha nchi ya nyumbani kwao na kwenda pamoja na familia yake katika nchi ya ugeni. Nchi hiyo ya ugeni aliyopewa Abrahamu ndiyo iliyokuwa nchi ya Wayahudi kwa nyakati hizo. Aliendelea kueleza jinsi Mungu alivyomwahidi Abrahamu kumpa mtoto ambaye angekuwa mtawala kwa nchi hiyo yote. Mungu akampa mtoto Isaka kama mtawala. Isaka akazaa mtoto na akamwita Yakobo, Yakobo akazaa watoto kumi na wawili ambao wakawa makabila kumi na mbili ya Israeli. Akazungumza kuhusu jinsi watoto wale walivyomuuza ndugu yao Josefu utumwani walipokuwa

wakielekea Misri. Mungu alikuwa pamoja na Josefu na akamfanya kuwa mmoja wa viongozi wakubwa wa Misri chini ya Farao. Kisha Mungu akamtumia Jesofu katika kuwaokoa ndugu zake kutokana na njaa kubwa iliyotokea.

Stefano akaendelea kuongea kuhusu jinsi Wayahudi walivyokuja kuwa na nguvu huko Misri, na jinsi Mungu alivyomwinua Musa ili kuwa kiongozi wao. Musa alikuwa ameua alipokuwa na miaka arobaini akimtetea Myahudi mwenzake. Na kisha akakimbilia msituni na Mungu akakutana naye katika kichaka kilichokuwa kikiwaka moto. Akiwa katika kichaka kile, Mungu alimwambia kile alichotaka akifanye. Musa akaanza kuwaongoza Waisrael. Ingawa si muda mrefu toka pale kwamba walianza kumwasi Mungu.

Waisraeli wakajitengenezea sanamu wakiwa jangwani, na ndipo Mungu akawaacha wakaanza kuabudu jua, mwezi na nyota. Stefano akaanza kuongea kuhusu hema ya ibada (tabernacle) walilotumia Wayahudi wakiwa jangwani katika kumwabudu Mungu. Akaongea kuhusu jinsi Wayahudi walivyomiliki nchi chini ya Joshua na kisha kustawi chini ya Daudi. Hatimaye Selemani akajenga hekalu kwa ajili ya Mungu, lakini Mungu hakujionyesha katika mahekalu yaliyojengwa kwa mikono ya wanadamu.

Baada ya kusema historia hii fupi juu ya Wayahudi, Stefano aliwakaripia viongozi wa Kiyahudi. Akawaambia kwamba mara zote walikuwa wamewakataa wafalme wa Wayahudi katika historia ya maisha yao, na sasa walikuwa wamemkataa na kumwua Yesu. Alipokwisha kusema hayo, watu walikasirika sana. Stefano akatazama juu na akapata maono juu ya Yesu akiwa amesimama mbinguni katika mkono wa kuume wa Mungu baba. Kisha Stefano akahutubia mkutano wa watu wote waliokuwa pale yale aliyoyaona katika maono yake. Alipokwisha kuwaeleza Wayahudi walimchukua Stefano mpaka nje ya mji na kumpiga kwa mawe mpaka kufa. Maneno ya mwisho ya Stefano yalikuwa, “Bwana usiwahesabie dhambi yoyote kwa kosa hili”, Na kisha akakata roho.

Maswali ya ufahamu

1. Kulikuwa na tatizo gani kanisani linaloonekana katika sura hizi?
2. Ni jinsi gani walivyotatua tatizo hilo?
3. Nini ilikuwa kazi ya watu wale saba?
4. Ni jinsi gani Stefano alijitetea aliposhtakiwa na Wayahudi kuwa alisema mambo kuhusu Musa na Mungu?
5. Nini kilitokea baada ya kujitetea kwa Stefano?
6. Ni maneno yapi aliyoyasema Stefano kabla ya kufa?

Ukweli wa kiroho:

1. **Watu wataumizwa katika hisia zao kanisani (Matendo 6:1).**

Katika somo lililopita tumeona kuwa dhambi iliingia kanisani. Katika somo hili tunaona kuwa kikundi kimoja cha watu walijisikia kutotendewa haki katika kanisa. Kama kanisa itakuwa muhimu kutambua kuwa watu wana mahitaji na hisia tofauti. Ingawaje, jukumu moja kubwa kama kanisa ni kubaki katika mshikamano na umoja. Mungu anataka kanisa lako kuwa na ushirika ulio imara kwa kila mmoja ili kuwa na umoja. Maombi ya mwisho ya Yesu Kristo yaliyomo katika maandiko kabla hajaenda msalabani ilikuwa ni katika

bustani ya Edeni (Yohana 17). Unafikiri aliomba juu ya nini – uinjilisti, waumini wengi, neno la Mungu kuenea? …. Hapana! Aliomba kwa ajili ya UMOJA miongoni mwa waumini. Litunze kanisa lako dhidi ya migawanyiko ya aina yoyote na uwe mwangalifu wakati mtu fulani anapokuwa hajisikii vizuri kuhusu kile ambacho kanisa linafanya. Usipuuzie malalamiko yake, mitume hawakupuuzia malalamiko ya watu wa Kiyahudi "Hellenists". Waliyashughulikia na kisha kutekeleza matakwa yao.

2. **Gawa madaraka (Matendo 6: 2 – 4).**

Mitume hawakuwa na muda wa kutimiza majukumu ya kazi zao na pia kuweza kuwahudumia wajane. Kwa hiyo waligawa madaraka hayo kwa watu saba waliokuwa waaminifu.

Mungu ataenda kuinua watu waaminifu mbali na mchungaji wako ambao wanaweza kuwa viongozi kanisani. Unapochagua viongozi, wajibu wako wa kwanza usiwe kufikiri kile watakachokifanya, lazima ufikiri jinsi kuwa wao ni akina nani. Kwa maneno mengine je watu hawa wanastahili na wana tabia zinazokubalika kuwa viongozi watumishi sambamba na mchungaji wako?

Makanisa mengi huwaita viongozi hawa WAZEE. Mzee anayestahili kuupokea wajibu huu kama mtumishi ili kusaidia kanisa, ufalme, na mchungaji wao. Biblia inatoa orodha katika 1 Tim. 3:8 – 13, juu ya baadhi ya tabia za mzee anayestahili. Kwa mfano, mbali na mambo mengine wazee lazima wawe wanaojali mambo muhimu, wasiwe wanafiki, wasiwe wenye kuzoelea vileo, na wasiwe wenye kupenda fedha lazima wawe watu wenye uzoefu, watu ambao wamehakikishwa. Pia kuna orodha ya mambo yanayotakiwa kwa wake zao. Kuwa mzee ni heshima kwa sababu kanisa linatambua kuchaguliwa kuwa ni watu wanaostahili. Ni heshima kuchaguliwa kuwa sehemu katika maisha ya utumishi.

3. **Mungu anatumia Agano la Kale na Jipya (Matendo 7:2 – 50)**

Stefano anatoa maelezo marefu kwa swali rahisi. Walimuuliza ikiwa alisema vitu juu ya Musa na sheria. Stefano alijibu akieleza juu ya Musa, Ibrahimu, hekalu, Joshua na vielelezo vingine kutoka Agano la Kale. Kama ni muumini mpya au kanisa jipya, huenda usielewe mambo mengi juu ya Agano la Kale. Ingawa, unaweza kuwa na uhakika kuwa kuna maelezo mengi katika Agano la Kale ambayo yanatufundisha kuwa Mungu ni nani na anafananaje. Anza kusoma Agano la Kale na kuelewa, hii itakufungua na kukupa uelewa mpana juu ya Bwana.

4. **Mungu haonekani katika mahekalu (Matendo 7:48)**

Katika Agano la Kale kulikuwa na Masinagogi na mahekalu, hizi ni sehemu ambazo Waisraeli waliweza kumwabudia Mungu. Israeli ikajisifu sana kutokana na sehemu hizi. Masinagogi na Mahekalu haya yalikuwa mazuri machoni pa wanadamu, lakini Mungu siyo kama sisi. Hahitaji jengo fulani ili aishi. Sehemu hizi za kukutumia zilikuwa nzuri kwa Waisraeli lakini hazikuwa za lazima kwa Mungu kuwepo pale. Biblia imejaa mifano ya Bwana akiwahudumia watu nje ya jengo lolote alilokuwa, kwa mfano, alikutana na Yakobo jangwani (Mwa. 28), Musa akiwa kichakani (Kutoka 3), na Mtume Paulo akiwa barabarani (Matendo 9).

Unapoanzisha kanisa, lazima uwe na shauku ya kuwa na jengo. Katika nchi, nyingi duniani hilo linawezekana. Ingawaje kama unataka jengo la kanisa omba kwamba hayo yawe mapenzi ya Mungu kwa ajili ya watu wa leo. Kumbuka kwamba tunapojenga jengo, hatujengi ili kumfanyia Bwana mahali pa kujihifadhi. Yeye hafungwi na sehemu. Tunajenga sehemu ya kukutanikia sisi wenyewe tu: sehemu ya kujisomea, ya burudani, kujumuika, pamoja na ibada.

Makanisa mengi mapya hayana pesa kwa ajili ya kujenga makanisa. Makanisa mengi mapya yanaona ni afadhali kutojenga kabisa. Mengine huchagua kutunza pesa na kujenga baadaye. Kama hauna pesa za kununua au kupanga jengo kutakuwa na sehemu zingine mnazoweza kukutana. Biblia inatuambia kuwa kanisa lilikutana katika nyumba za watu (Matendo 16: 40, 17: 5,6: 18:7), katika shule (Matendo 19:9) na pia hadharani na kutoka nyumba kwa nyumba (Matendo 20:20). Mwombe Mungu akuonyeshe mahali pa kukutana.

5. **Mateso yapo na mwitikio wako ni wa maana.**

Stefano ni mtu aliyekuwa amejawa na Roho Mtakatifu. Alikuwa mtu mzuri, mcha Mungu. Ingawaje, hakuweza kuwa huru katika kuyaepuka mateso. Na hatimaye Stefano akauawa kwa ajili ya imani yake. Katika sehemu nyingi duniani Wakristo hukutana na mateso kama kanisa kwa ajili ya imani zao. Yesu Kristo mwenyewe alituonya kwamba tutakutana na matatizo katika dunia hii. (Mt. 6:34). Kama hivi ndivyo katika maisha yako, basi uwe na imani kuwa mateso tunayoyapata hapa ni kama daraja tu la kuufikia ule utukufu tunaoutarajia kule mbinguni. (Efe. 1:18). Mungu anaweza kutumia mateso katika kuwaleta wengine kwake. Mwitikio wa Stefano wa upendo na msamaha kwa wale waliomchukia, “Bwana usiwahesabie dhambi hii” na hii lazima ilitenda kazi ya mabadiliko katika moyo wa Sauli. Sauli ambaye baadaye alikuja kujulikana kama mtume Paulo na akiwa mmoja wa mitume wakubwa na mwanzilishi wa makanisa ambaye hajawahi kutokea.

Katika somo linalofuata tutaangalia lilivyoenea kwa watu wa aina na mataifa mbalimbali. Tutaona jinsi matendo ya kanisa lile la kwanza tunavyoweza kuyahusisha na makanisa yetu leo.

Viongozi wa kanisa walieneza Neno (Ubatizo na meza ya Bwana) Matendo 8

Mstari mkuu “…Ni nini kinanizuia nisibatizwe? Kisha Filipo akasema, “Kama ukiamini kwa moyo wako wote unaweza”. Matendo 8: 36b – 37.

Maswali ya ufahamu.

1. Nini kilitokea katika siku ya Pentekoste? Je watu wote waliokuwa wamekusanyika waliamini?
2. Lielezee kanisa baada ya watu wengi kuamini katika siku ya Pentekoste?

3. Ni nani aliyeponya kati ya Petro au Yohana pale hekulani? Mwitikio wa makuhani ulikuwa upi?
4. Anania na Safira walikuwa akina nani?
5. Stefano alikuwa nani na alikufaje?
6. Madhumuni matatu ya kanisa ni yapi?
7. Ni kwa jinsi gani Mungu kwa jumla anajifunua na mapenzi yake kwetu leo?

Sauli aliridhia kuuawa kwa Stefano. Wakati huo kanisa lilianza kuteswa. Waumini wakatawanyika kote Uyahudi na Samaria isipokuwa mitume ndio walioweza kubaki Yerusalemu. Sauli akaanza kulitesa kanisa, akiingia kila nyumba na kuwapeleka waumini katika gereza.

Wale ambao walitawanyika wakaanza kueneza neno la Kristo. Mmoja wa wale saba akachaguliwa na mitume, Filipo akaenda katika mji wa Samaria na akaanza kuhubiri injili kwa wenyeji wa pale. Wengi wakampokea Kristo, mapepo wengi yakakemewa na watu wengi wakafunguliwa, kukawa na furaha kuu katika mji huo.

Kulikuwa na mtu katika mji huo aliyekuwa anafanya mambo ya ushirikina aitwaye Simoni. Akiwa mshirikina alikuwa ameuogopesha mji wote katika yale aliyokuwa akiyatenda. Ingawaje, baada ya mji huo kuanza kumgeukia Kristo, Simoni mshirikina pia aliamini na kubatizwa. Alishangazwa na ishara na miujiza ambayo Filipo aliitenda kwa jina la Yesu.

Mitume wakasikia kuwa Wasamaria walikuwa wamemwamini Kristo. Petro na Yohana wakaja kuchunguza kilichokuwa kinaendelea. Walitaka kuwawekea mikono wale waumini wapya ili kwamba wao pia wapokee Roho Mtakatifu. Hakuna hata mmoja wao ambaye alikuwa amempokea Roho Mtakatifu. Simoni akaingiwa shauku ya kutaka kufanya kile ambaho mitume walikuwa wakifanya. Akitoa fedha ili wampe na yeye uwezo wa kuwawekea mikono na kupokea Roho Mtakatifu. Petro akamwambia haiwezekani pesa yako yaweza kufa pamoja naye. Petro akamkemea na kumtaka atubu kwa ajili ya fikira hizo mbaya. Baada ya Petro kusema haya Simoni akamwomba amwombee ili jambo lolote baya katika aliyoyasema lisimpate. Petro na Yohana wakahubiri neno la Bwana, wakarudi Yerusalemu wakihubiri katika vijiji vingine vingi vya Wasamaria.

Kisha malaika akamtokea Filipo na kumwabia kwenda katika ile barabara ya jangwani ili kukutana na mtu kutoka Ethiopia. Huyu alikuwa ni mtu maarufu, towashi aliyefanya kazi kwa malkia wa Ethiopia. Alikuwa mkubwa wa watunza fedha wote. Alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu. Akiwa njiani kurudi, alikuwa akisoma katika kitabu cha nabii Isaya. Malaika akamwambia Filipo kuipita ile gari.

Filipo akamuuliza yule towashi kama alikuwa anaelewa alichokuwa anakisoma. Yule Mwethiopia akajibu “Nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza?” kwa hiyo Filipo akaanza kufafanua sehemu hii pamoja na habari za Kristo katika maisha yake. Kisha yule Mwethiopia akasema, “Tazama hapa kuna maji, ni nini kinanizuia nisibatizwe?” Filipo akajibu, “kama ukiamini kwa moyo wako wote yawezekana” naye akasema naamini ya

kuwa Yesu Kristo ndiye mwana wa Mungu, akaamuru lile gari lisimame Filipo akatelemka chini na yule towashi na kumbatiza. Walipokuwa wakitoka majini, Filipo akachukuliwa na Roho wa Bwana katika mji ulioitwa Azoto na kutoka pale akaendelea kuhubiri kijiji hadi kijiji mpaka alipofika Kaisaria.

Maswali ya ufahamu:

1. Nani aliyeanza kulitesa kanisa?
2. Ni nani waliotawanyika katika nchi na ni waumini wapi walibaki Yerusalemu?
3. Filipo alienda wapi kuhubiri injili? Mwitikio wa watu ulikuwaje?
4. Kwa nini Petro na Yohana walienda Samaria?
5. Ni nini ambacho Simoni alitaka kununua?
6. Nani aliyemfanya Mungu amwongoze Filipo kumshuhudia katika jangwa.
7. Ni nini alichokifanya yule towashi wa Ethiopia baada ya kusikia ujumbe wa Kristo?

UKWELI WA KIROHO

1. **Uwahubiri wale waliokataliwa (Matendo 8:5)**

Filipo alikuwa Myahudi. Kwa Myahudi ilikuwa vigumu sana kufanya kazi na Wasamaria. Wasamaria hawakuwa Wayahudi halisi katika kuzaliwa, walikuwa mchanganyiko na watu wa mataifa (ambao siyo Wayahudi) katika maisha yao na vile vile katika mambo ya dini. Wayahudi waliwaona Wasamaria kuwa ni watu wa chini na hawakutaka kushiriki nao katika jambo lolote. Ingawa kwa upendo wa Kristo na nguvu za Roho, Filipo alikwenda kumshuhudia Msamaria kuhudu Kristo. Alitupilia mbali chuki ili kumwongoza Msamaria katika imani. Ikiwa unasoma habari hizi ukiwa Afrika, Marekani ya Kusini, Marekani ya Kaskazini au Ulaya, sisi sote tunawafahamu watu ambao tunakuwa na wakati mgumu kuwa pamoja nao. Labda ni watu kutoka mji karibu na sisi au kijiji. Labda ni watu wa kabila tofauti na letu au mazingira. Kwa hali yoyote Mungu anakutaka ushirikiane nao. Hili ni jambo la muhimu katika UINJILISTI. Tutajadili hizi kanuni za uinjilisti katika masomo yanayofuata. Ingawaje, kwa wakati huu muanze kufikiri kama kikundi iwapo kuna watu ambao mnaona shida kuwaambia habari za upendo wa Kristo. Kama hamna upendo wa kutosha kuwaambia habari njema za Kristo, muombe Mungu awape upendo huo.

2. **Wanafunzi wako wanaweza kukukatisha tamaa (Matendo 8:9 – 25)**

Filipo alimsaidia mtu aliyekuwa maarufu aliyeitwa Simoni kufanya uamuzi wa kumpokea Kristo. Kuna mijadala mingi iwapo kweli Simon aliamini au siyo. Ingawa, bila shaka hakuna mjadala kwamba Filipo alifikiri kwamba alikuwa ameamini. Baada ya Petro na Yohana kuanza kufanya maajabu kule Samaria, ilionekana wazi kuwa Simon alijihusisha na vitu ambavyo havikuwa sawa na alitaka kununua “nguvu” kutoka kwa Petro na Yohana. Ni dhahiri kuwa unapoanza kuwashuhudia wengine habari za Kristo, watu unaowaongoza kwa Kristo watafanya makosa (wanafunzi wa Yesu walifanya).

Baadhi ya watu unaoshirikiana nao na kuanza kushuhudia wanaweza kukushangaza na pengine wasiwe waumini wa kweli. Lakini hilo haliwezi kuwa msamaha wa kuacha kufanya uinjilisti. Makosa ya Simoni hayakumfanya Filipo kuacha. Kumbuka kwamba

baada ya Samaria Filipo alisaidia kumshuhudia towashi wa Ethiopia na akaendelea katika miji mingine akiendelea mpaka Kaisaria.

3. **Kristo hakuenda upande wa "Magharibi" (Matendo 8: 26 – 40)**

Watu wengi wanadhania kuwa Ukristo kimsingi ni wa watu wa Magharibi tu (Ulaya na Marekani). Ingawaje, baada ya Mungu kuanza kueneza habari njema za Kristo kwa Israeli, sehemu ya kwanza ambako injili ilikwenda ni Afrika, isitoshe, yule towashi wa Ethiopia alikuwa mtu mashuhuri huko Afrika ya Kaskazini. Na kwa wakati huu injili ilienea katika sehemu mbalimbali, lakini ni ajabu kuona kwamba Mungu ameiweka Afrika katika Biblia kama sehemu ya kwanza iliyoonyeshwa kuwa injili ilielekea na kuenea kwanza. Hivyo, kumfuata Kristo siyo kufuata dini ya watu weupe au watu wa Magharibi. Kristo anajenga kanisa lake katika mataifa yote.

4. **Mungu ametupa maagizo mawili kama kanisa (Matendo 8:38).**

Katika somo hili tumejifunza kwamba nguvu ya kanisa inatoka kwa Roho Mtakatifu. Tumejifunza kwamba msingi wa huduma yetu ni maombi. Tumejifunza kwamba kanisa lazima liwe na shauku ya kujisomea maandiko kwa sababu huo ndio ufunuo kwa ujumla ambao amejidhihirisha kwetu. Tumejadili madhumuni matano ya kanisa lako jipya – maombi, ibada, ushirika, huduma na kufuasa.

Lakini pia Mungu anatoa maagizo mawili kwa kila kanisa, kwa kila nchi, kwa kila karne, kuzifuata Mungu ameagiza kila kikundi cha waumini kufanya UBATIZO na MEZA YA BWANA.

Ubatizo – Filipo alifanya uinjilisti kwa towashi wa Ethiopia. Alimwambia kuwa kama angemwamini Yesu kuwa ni mwana wa Mungu angeweza kubatizwa. Yule towashi akaamini na akabatizwa pale pale.

Ubatizo ni ishara ya uamuzi wetu wa kumpa Yesu maisha yetu. Hii siyo sehemu muhimu katika wokovu (1Wakorintho 1:17), lakini ni tendo la muhimu la kuonyesha kutii kwetu baada ya kuyatoa maisha yetu kwa Yesu. Muumini anapozamishwa majini (katika bwawa dogo, ziwani, baharini n.k.) na kisha anatolewa nje tena, hii inatoa ishara kifo cha mtu huyo na kuzikwa kwa dhambi yake ya asili (ya zamani) na kufufuka ili kutembea katika maisha mapya pamoja na Yesu Kristo.

Kama kanisa unatakiwa kuanza kufanya ubatizo, lini? Sasa ndio wakati wa kuanza. Kama una watu kanisani kwako ambao wamempokea Kristo, lakini hawajabatizwa, basi wanahitaji kubatizwa. Biblia inaonyesha kwamba ubatizo ulifanyika mara moja baada ya kuamini (Matendo 9:38, 2:38 – 41). Baadhi ya makanisa wanajisikia kuwa na madarasa ya walioamini kabla ya kuwabatiza ili kuona udhabiti ya kuamini kwao. Kanisa lako lahitaji kuamua ni utaratibu upi utatumika kabla ya ubatizo, uwe mwangalifu kutoongeza mambo yasiyokuwemo katika maandiko. Sharti moja kuu kwa ubatizo ni kwamba, je ametubu na kumpa Yesu moyo wake?

Nani abatize? Tunaona kuwa wanafunzi walibatiza (Yohana 4:1–12) Mwinjilisti Filipo alibatiza (Matendo 9:38), na wanafunzi fulani walibatiza (Matendo 9:10). Kanisa lako liamue nani atabatiza. Ubatizo unafanyika chini ya mamlaka ya Kanisa. Ingawa,

kumbuka kwamba Filipo hakuwa mchungaji, alikuwa mwinjilisti tu ambaye aliteuliwa na kanisa. Katika maandiko hakuna ilipoonyeshwa kuwa ni wachungaji tu ndio walioweza kubatiza.

Meza ya Bwana – Hili ni agizo la pili ambalo sisi kama kanisa ametuagiza tulifanye. Meza ya Bwana ni njia ya kanisa kukumbuka kifo cha Yesu msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. tunashiriki mkate na mvinyo ili kutoa ishara ya mwili na damu ya Yesu. Hakuna ishara yoyote katika maandiko kwamba mkate na mvinyo hasa hugeuka kuwa mwili na damu ya Yesu halisi kama baadhi ya makanisa hapa duniani yanavyofundisha. Hakuna ishara yoyote ambayo inaonyesha kuwa ni lazima ushiriki ushirika mtakatifu ili kupokea neema ya wokovu kama baadhi ya makanisa yanavyofundisha. Isitoshe, kama tunahitaji mara kwa mara kupokea neema ya wokovu, wiki baada ya wiki basi kifo cha Yesu msalabu hakikutosha kwa ukombozi wetu (Waebrania 7:27). Kufa kwake mara moja msalabani kunatosheleza msamaha na neema katika maisha yetu. Hatuhitaji kupokea neema kutoka katika kitendo au sharti fulani.

Kama unapenda kuona jinsi ambavyo Kristo alifanya chakula cha Bwana au ushirika Mtakatifu, unaweza kusoma sehemu zifuatazo katika maandiko (1Korintho. 11:17–26, Mt. 26: 26–29, Marko 14: 22–25, Luka 22: 19–20) Maandiko haya yatakusaidia kuamua ni njia gani utaitumia katika kanisa lako mnaposhiriki mkate na mvinyo kukumbuka kifo cha Kristo pale msalabani. Katika wiki zinazofuata mshiriki pamoja chakula cha Bwana. Soma alivyofanya Yesu tena katika Mathayo, Marko, Luka na 1 Wakorintho. Andaa mkate na mvinyo (au juisi ikiwezekana) na uwashauri waumini wote kujiandaa. Kumbuka kusoma wosia wa Paulo katika 1 Wakorintho 11: 27–34. Jiandae kiroho kabla ya kunywa mvinyo na kula mkate. Tubu dhambi zako kwa Mungu ili kwamba ukumbuke sadaka ya mwanawe Yesu katika mtazamo na roho iliyo sawa. Kumbuka kuwa ni wale waumini tu wanaotakiwa kula chakula cha Bwana.
Mara kwa mara kumbuka kuadhimisha chakula cha Bwana pamoja kama kanisa. Jadilini, kama kanisa, jinsi mtakavyokuwa mnafanya.
Katika somo linalofuata tutaangalia viongozi wawili kati ya viongozi wakuu wa kanisa la kwanza. Somo litatuonyesha jinsi walivyolihusisha dhumuni la sita la kanisa katika maisha yao.

SOMO LA 7.
Mmisionari mkubwa wa kanisa anaokoka
(Uinjilisti)
Matendo 9

Mstari Mkuu: “Mara akamhubiri Yesu katika masinagogi, kwamba yeye ni Mwana wa Mungu” (Matendo 9:20)

Maswali ya ufahamu:

1. Ni jinsi gani Kristo alirudi mbinguni?
2. Ni nini kilitokea katika siku ya Pentekoste?
3. Nani alienda hekaluni kuomba? Kilitokea nini pale?
4. Ni nini madhumuni manne ya kanisa?
5. Dhambi ya Anania na Safira ilikuwa nini?
6. Kilitokea nini kwa Stefano?
7. Ni nani aliyechukua mavazi wakati wa kuuawa kwa Stefano?
8. Nani alimshuhudia Msamaria? Kwa nini ilikuwa vigumu hivyo?
9. Nani alimfanya yule towashi wa Ethiopia kuja kwa Kristo?

Saulo aliendelea kulitesa kanisa. Aliomba ruhusa kwa kuhani mkuu aende Dameski ili kuwaweka waumini katika gereza, akiwa njiani kwenda Dameski, akaona nuru kubwa. Akaanguka chini na akasikia sauti ikisema, ‘Sauli Sauli mbona unaniudhi?” Sauli akauliza ni nani wewe unayesema, na Bwana akajibu akisema ni Yesu. Sauli akatetemeka sana, na akamwomba Bwana, “Bwana unanitaka nifanye nini?” Bwana Yesu akamwambia aende katika mji na asubiri. Watu waliokuwa wanasafiri na Sauli walisikia sauti lakini hawakuelewa. Sauli akazinduka kutoka ardhini, lakini hakuweza kuona. Wafuasi wake wakamsaidia kumpeleka katika mji ule. Akasubiri kwa muda wa siku tatu. Kwa siku zile zote hakuweza kuona, na pia hakula au kunywa.
Hatimaye Mungu akaongea na mtu aliyeitwa Anania. Akamwambia aende kwenye mtaa ulioitwa mnyofu. Akamtafuta Sauli aliyekuwa akiomba na kumsaidia apate kuona tena. Anania hakutaka kwenda alikuwa amesikia mengi juu ya Sauli na alivyokuwa amewatendea Wakristo. Mungu akamhakikishia Anania kuomba ilimpasa aende kwa sababu makusudi ya Mungu kwa Sauli yalikuwa kupeleka injili kwa mataifa, wafalme na kwa wana wa Israeli. Ingawaje, Mungu alitaka amuonyeshe Sauli ilivyompasa kuteseka kwa ajili ya ufalme kwanza. Anania akamtii Bwana na akafika katika nyumba ambayo Sauli alikaa. Akamwekea mikono ili kwamba apate kuona tena. Ghafla vikaanguka vitu kama magamba machoni pake. Akapata kuona tena. Akasimama na akabatizwa. Baada ya hapo Sauli akala chakula na akapata nguvu, akawa huko siku kadha wa kadha pamoja na wanafunzi walioko Dameski.

Mara akaanza kumhubiri Yesu katika masinagogi ya Kiyahudi kila mtu alishangazwa kwa sababu walijua ni nini Sauli alichokuwa amelifanyia kanisa kabla ya hapo. Mungu akaanza kumtumia Sauli kuwaonyesha watu wengi kwamba Yesu ni Kristo. Mapema baada ya kusikia, Wayahudi wakapanga njama za kumuua Sauli. Kwa hiyo wanafunzi wa Dameski wakaanza kumsaidia Sauli, wakamtwaa usiku wakamshusha ukutani, wakimtelemsha katika kapu kubwa chini ya ukuta wa mji.

Kisha Paulo alitoka kuwasalimu wanafunzi kule Yerusalemu, lakini walimwogopa. Kwa hiyo Barnaba akamleta Yerusalemu na akaongea badala yake kwa mitume. Sauli akaenda kwa wanafunzi na akafananisha habari ya kuokoka kwake akiwa njiani kwenda Dameski na jinsi alivyohubiri kwa nguvu katika mji ule.

Kwa hiyo Paulo akabaki Yerusalemu na akaendelea kuhubiri neno, lakini mapema Wayahudi wakaanza kupanga kumwua. Sauli akarudi Kaisaria na kisha Tarso. Makanisa yakaanza kukua na kustawi.

Huduma ya Petro ilikuwa inaendelea katika kipindi hiki. Alipokuwa akielekea Israeli akamponya mtu aliyepooza akatembea tena. Pia alimsaidia mwanafunzi mwema aliyeitwa Dorkasi. Dorkasi alikuwa ni mtu aliyekuwa ametenda matendo mengi mema. Alifariki na rafiki zake wakampeleka kwa Petro ili kupata msaada, Petro akafika na akamwamuru Dorkasi ainuke, akazinduka kutoka katika wafu na mapema watu wengi katika mji ule wakamwamini Bwana. Baada ya tukio hili, Petro akakaa siku kadha wa kadha katika mji wa Yafa nyumbani mwa mtu mmoja jina lake Simoni, mtengenezaji wa ngozi.

Maswali ya ufahamu:

1. Sauli alikuwa nani?
2. Ni mji gani aliokuwa anaenda kuwatesa waumini?
3. Ni nini kilitokea akiwa njiani kwenda Dameski?
4. Nani alikuja kumsaidia Sauli ili aone tena?
5. Ni nini alichofanya Sauli baada ya kuona tena?
6. Je waumini wa Yerusalemu walitaka kuonana na Sauli?
7. Bwana aliwaponya watu wawili kupitia Petro katika habari hii, ni akina nani hao?

Ukweli wa kiroho.

1. Baadhi ya watu waliokuwa wagumu sana walikuja kuwa miongoni mwa viongozi wakubwa katika kanisa (Matendo 9:1 – 19).

Wakati mwingine ni rahisi kuangalia aina fulani ya watu na kufikiri kuwa kamwe hawawezi kumpokea Kristo. Isitoshe, tumwangalie Sauli. Alikuwa mwangamizaji wa Wayahudi. Alikuwa amefundishwa katika shule zote nzuri za Kiyahudi. Alikuwa mtesaji mkuu wa Wakristo. Aliwatupa Wakristo wengi katika jela. Pia alishuhudia viongozi wenzake wa kidini walipokuwa wakimwua mtu wa kwanza kufa kwa ajili ya Kristo – Stefano. Iliwezekanaje mtu kama huyo kuja kwa Kristo? Ingawaje, Kristo alikuwa na mpango na maisha ya Sauli. Alijifunua kwa Sauli akiwa njiani, na Saulo ambaye baadaye akaja kujulikana kama mtume Paulo) akabadilishwa maisha yake na kumpa Yesu.

Kuna watu katika mji wako wanaoonekana kuwa mbali sana na habari za kuokoka, lakini usipoteze matumaini; Mungu bado ana mpango kwa ajili yao. Mmisionari mmoja aliniambia, “Ninawaangalia wale watu ambao ni wagumu kuisikia injili, wanaweza kunifanya kuwa mtume Paulo wa pili”. Unapofanya uinjilisti, kanisa lako lazima kwanza watafute wale watu wanaoonekana kuwa rahisi kupokea injili. Mungu anaweza kuwa tayari amekwishafanya kazi katika mioyo yao. Kisha inabakia kazi ya kuchagua tu

matunda ambayo tayari Mungu ameyaandaa. Lakini kwa wakati huo huo omba kwamba Mungu akuonyeshe waume na wanawake ambao wanaonekana wako mbali sana na injili. Inawezekana hao watu wanaoonekana kuwa wagumu ni viongozi wa makabila au wanawake wafanya biashara au wakufunzi katika vyuo vikuu ambao wanaweza kuwa wahubiri wa injili wenye nguvu. Usitupilie mbali kuwaambia kuhusu imani vile vile.

2. UINJILISTI – Madhumuni sita ya kanisa (Matendo 9: 20 – 43).

Tumekwishaona juu ya maombi, ibada, ushirika, huduma na uanafunzi. Leo somo hili tutaangalia juu ya UINJILISTI. Mchungaji mkubwa kwa jina la Rick Warren aliwahi kusema kuwa madhumuni mengine ya kanisa tutayafanya milele. Tutamwabudu Bwana mbinguni. Tutakuwa na ushirika na Wakristo wengine. Tutahudumu mbinguni. Tutakua katika ufahamu wa Baba (Mamilioni na mamilioni ya miaka huko mbinguni tutakuwa na muda wa kutosha kujifunza zaidi juu yake). Lakini hatutafanya uinjilisti pale, hatutawaambia wengine kuhusu Kristo. Mbinguni, tutakuwa tumechelewa kuwaambia wengine habari za Kristo.

Kazi ya uinjilisti kwa kanisa ni ya muhimu sana. Moyo wako wa uinjilisti kama kanisa utakusaidia kujitambua wewe utakuwa kanisa la namna gani. Itakusaidia katika kuunda kanisa ambalo ama linalenga katika mahitaji yake tu, au kanisa ambalo mara zote linatoka nje na kuangalia mahitaji ya kiroho ya wale wanaolizunguka. Uinjilisti pia unaweza kuwa kitu kigumu sana kati ya madhumuni yote. Kwa mfano, madhumuni mengine yote ya kanisa yanaweza kufanywa na watu miongoni mwa washiriki. Unaweza kuwa na ushirika miongoni mwenu, kufanya wanafunzi pamoja, kuabudu pamoja, na kuhudumiana kila mmoja (na vile vile kwa watu wengine). Lakini uinjilisti siku zote unafanyika kwa wale waliopotea, na hivyo inaweza kuwa ngumu sana. Kufanya uinjilisti ipasavyo, waumini wawe wazi, wawe na urafiki, na kuwa tayari kuhatayarisha maisha kama Kristo alivyofanya kwa ajili yetu alipowashuhudia watu ambao pengine hawakuwa tayari kusikia habari njema. Hili ni suala linaloogopesha. Kwa sababu hiyo, makanisa mengi yanaacha dhumuni hili.

Lakini kanisa katika Matendo ya Mitume halikuacha kutumiza dhumuni la uinjilisti. Katika sura hii wawili kayi ya viongozi wao Petro na Sauli walienda nje wakihubiri injili. Isitoshe Sauli alianza kumhubiri Kristo mara tu baada ya kuokoka na kuweza kuona tena (Matendo 9:20). Petro alikuwa nje akisafiri katika Israeli na kupitia matendo yake aliweza kuhubiri injili na mji wote wakasikia habari za Yesu (Matendo 9:35, 42). Uinjilisti ulianzishwa na viongozi wa kanisa.

Lakini siyo viongozi tu, lakini waumini wote wameitwa kwa kazi ya uinjilisti. Katika somo la wiki iliyopita tumekwishaona jinsi Filipo alivyoshuhudia imani yake. Katika somo la pili tulijifunza kwamba baada ya Pentekoste, kanisa lilikua siku hadi siku (2:47) na tunaona kuwa watu walijiandaa kupitia Roho kulihubiri neno kwa nguvu (Matendo 4:31). Washuhudiaji wa kila siku wakaongezeka kwa wingi kiasi kwamba injili imeweza kufika mlangoni kwako leo. Kanisa lako lazima lijengwe katika msingi kwamba litakuwa la mtazamo wa uinjilisti. Tokea mwanzoni lazima uwe na shauku ya kufanya uinjilisti kwa waliopotea ili kuanza mchakato wa kufanya wanafunzi kwa ajili ya ufalme wa Mungu.

Uinjilisti ufanyike vipi? Kuna njia nyingi za kuishuhudia imani. Kama unahudhuria somo hili, huenda umetumia moja kati ya mtiririko wa masomo ya uinjilisti uvumbuzi kama ile “Habari njema za Yesu”au “kuanza maisha mpaya na Kristo”. Masomo haya ni mazuri sana kama unataka kumsaidia mtu kujisomea Bibli ili aweze kumshuhudia Kristo. Zinakuongoza hatua kwa hatua jinsi unayoweza kumwongoza mtu katika yale masomo ya saba na nane ya Neno la Mungu. Kama huna masomo haya, au mengine yoyote yale yanayofaa kujisomea kwa ajili ya uinjilisti, hapa kuna njia zingine mbili rahisi za kuwashuhudia wengine.

Njia ya kwanza ni kuwashirikisha ushuhuda wako. Ushuhudia ni maneno mafupi kuhusu jinsi ambavyo Kristo alibadilisha maisha yako. ninapowashirikisha ushuhuda wangu, ninapenda kuuugawa katika sehemu kuu tatu.

1. Maisha yangu kabla ya kumpokea Kristo
2. Jinsi nilivyoyatoa maisha yangu kwake
3. Maisha yangu pamoja na Kristo sasa

Ninachukua dakika moja au mbili kwa kila sehemu na kuielezea jinsi maisha yangu pole pole yalibadilishwa na Kristo. Baada ya kufanya hivi, ninapenda kuwashirikisha wao pia wanavyoweza kuyatoa maisha yao kwa Kristo. Chukua dakika chache za kufanya mazoezi jinsi utakavyowashirikisha sehemu hizi tatu. Kumbuka, ufanye kuwa mfupi (dakika 5) na uwe rahisi. Acha Roho Mtakatifu akuongoze.

Njia ya pili inaitwa Barabara ya Kirumi. Hii ni mistari sita ambayo unaweza kuitumia kuishuhudia imani kwa dakika chache tu na kuonyesha ni kwa nini mtu anaweza kumgeukia Kristo. Mistari hii ni kama ifuatavyo:-

1. 1 Yohana 5:13 – mstari huu unaonyesha kwamba neno la Mungu liliandikwa kukuonyesha jinsi ya kupata wokovu.
2. Warumi 3:23 – mstari huu unaonyesha kwamba sote tu wenye dhambi
3. Warumi 6:23 – mstari huu unaonyesha hukumu ya Mungu kwa dhambi
4. Warumi 5:8 – mstari huu unaonyesha kuwa Mungu alimtuma Kristo kufa kwa ajili yetu.
5. Warumi 10:9–10 mistari hii inaonyesha tunachotakiwa kufanya ili kumpokea Kristo, na kumwita kama Bwana (kujitoa kwake)
6. Warumi 10: 13 – mstari huu unaonyesha kwamba mtu yeyote anaweza kuja kwa Kristo.

Kama kanisa chukua dakika 10 – 30 kusoma mistari hii ongea jinsi unavyoweza kueleza kila mstari kwa rafiki zako. Tafadhali kumbuka kwamba unaposhuhudia, usiogope kwamba yote utakayosema yatakuwa sawa. Biblia inatuahidi kwamba Roho Mtakatifu atatuongoza katika kusema (Luka 12:12, Yohana 14:26, 16:13), Mungu amekuchagua tu kama chombo cha kupeleka Habari Njema kwa mtu fulani. Ikiwa unasaidia kufanya uinjilisti kwa dunia iliyopotea, utakuwa miongoni mwa kikundi cha watu waliosaidia kueneza upendo wa Kristo kutokea wakati wa kufufuka kwake mpaka sasa.

Katika somo la mwisho, tutaona jinsi watu wa mataifa hatimaye walivyoweza kufikiwa na habari za Kristo na kwamba hii ina maana gani kwako leo.

SOMO LA 8

Kanisa linapata maono kwa ajili ya ulimwengu
(Utume)
Matendo 10 – 13

Mstari mkuu: Kisha Petro akapaza sauti akisema, “Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo, bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye”. Matendo 10: 34,35.

Maswali ya ufahamu:

1. Nini kilitokea siku ya Pentekoste?
2. Eleza jinsi kanisa la kwanza lilivyokutana kutendeana kwa kila mmoja?
3. Nini kilitokea wakati Petro na Yohana walipoenda kuomba hekaluni?
4. Kwa nini Anania na Safia walikufa?
5. Ni jinsi gani mitume walishughulikia tatizo la kuwatunza wajane?
6. Stefano aliwatendea vipi wale waliomponda kwa mawe?
7. Alikuwa wapi yule towashi ambaye Filipo alimshuhudia?
8. Madhumuni matano ya kanisa ni yapi?
9. Msingi wa huduma yetu uwe nini?
10. Tusome nini ili kujua Mungu ni nani na makusudi yake katika maisha yetu ni yapi?

Kulikuwa na mtu jina lake Kornelio ambaye alikuwa kiongozi katika jeshi la Kirumi. Alikuwa mwenye juhudi akimwomba Mungu siku zote na alikuwa mtu mwema kwa Wayahudi. Siku moja saa tisa kamili mchana, malaika akamtokea akiwa katika kuomba. Malaika akamwambia kwamba maombi yako yamejibiwa na kwamba amwite Petro ambaye alikuwa Yafa ili aje kwake.

Kwa hiyo Kornelio akawatuma watu waaminifu kumfuata Petro. Siku iliyofuata Petro alikuwa akiomba majira ya saa sita mchana. Akapata hasira nyingi na alipokuwa akisubiri chakula akaingiwa na usingizi mzito. Akapata maono kwamba mbingu zimefunguka na chombo kinashuka kama nguo kubwa inatelemshwa toka mbinguni kwa pande zake nne. Nikaona wanyama wa nchi wenye miguu minne, na wanyama wa mwitu, nao watambaao na ndege wa angani, yaani wale najisi na wasio najisi kulingana na sheria ya Kiyahudi. Kisha sauti ikaniambia kuwaua na kuwala wanyama. Petro akamwambia Bwana kwamba asingeweza kufanya hivyo sababu asingeweza kula wanyama wasio safi (walio najisi). Bwana akamwambia kwamba alichokitakasa, Petro hawezi kukiita najisi. Jambo hili lilitendeka mara tatu.

Petro alikuwa bado akifikiri maana ya ndoto ile wakati watu wa Kornelio walipofika mlangoni. Wakamwulizia Petro na akaja kuwasalimia. Wakamwambia kuwa malaika amemwambia Kornelio kuwaita. Petro akawakaribisha kwake usiku ule. Siku iliyofuata wakaenda kwa Kornelio.

Siku iliyofuata Petro, marafiki wengine wa Kiyahudi pamoja na watumishi wa Kornelio wakafika Kaisaria. Kornelio alikuwa amewaalika ndugu zake pamoja na marafiki wa karibu kuwa pamoja. Walikuwa nyumbani kwake wakimsubiri Petro. Alipofika Petro Kornelio alianza kupiga magoti na kumwabudu. Petro akamwambia Kornelio kuinuka

kwa sababu isitoshe Petro alikuwa kama yeye Kornelio tu. Kisha Petro akamwambia kuwa kama Myahudi hakuruhusiwa kujihusisha na mtu yeyote wa taifa jingine, lakini Mungu akamwonyesha kuwa asimwite mtu yeyote najisi. Kisha akaja nyumbani kwa Kornelio na hali ya kupingana na Bwana. Petro akaanza kuhubiri kuhusu Kristo. Akisema kuwa mitume wote waliaminiwa kuhubiri kuhusu msamaha wa dhambi kwa wale wanaomwamini Kristo. Alipokuwa anasema haya Roho Mtakatifu akaifunika nyumba ile. Wayahudi wote waliosafiri pamoja na Petro wakashangazwa kwamba watu wa mataifa walikuwa wamempokea Roho Mtakatifu kama wao walivyokuwa wamempokea. Petro akaamuru kuwa mwenye nyumba ile abatizwe. Kisha Petro pamoja na wenzake wakabaki pale kwa siku zingine kadha wa kadha.

Baadhi ya waumini wa Kiyahudi katika Yerusalemu walikasirika sana sababu Petro alibaki kukaa na watu wa mataifa. Petro akawaeleza yote yaliyotokea. Akawaambia jinsi Bwana alivyotuma maono ya wanyama katika kitu kama nguo na kisha jinsi alivyotakiwa kwenda katika nyumba ya Kornelio. Aliwaambia jinsi alivyoanza kuhubiri injili na kisha jinsi Roho Mtakatifu alivyokuja kwa waumini wapya wa mataifa.

Aliwaambia jinsi alivyokumbuka maneno ya Yesu Kristo alivyowafundisha juu ya Roho Mtakatifu. Petro alisema kuwa kama Mungu amechagua kuwapa kipawa kile kile watu wa mataifa ambacho amewapa Wayahudi, iliwezekanaje kupingana na Mungu? Wayahudi waliposikia haya, wakamtukuza Mungu kwa kuwa alikuwa amewapa watu wa mataifa toba kwa ajili ya uzima wa milele.

Baada ya kifo cha Stefano wengi wa wafuasi wa Kristo walienda katika nchi za jirani wakimshuhudia Kristo kwa Wayahudi. Baadhi yao wakaenda katika mji ulioitwa Antiokia huko Siria na wakaanza kuwashuhudia Wagiriki. Watu wengi katika mji ule wakampokea Kristo. Waumini huko Yerusalemu wakasikia juu ya hili na wakamtuma Barnaba kwenda kujua kilichokuwa kinaendelea. Barnaba akamchukua Sauli na wakaenda Antiokia. Wakawafundisha waumini wa Antiokia kwa mwaka mmoja na wanafunzi kwa mara ya kwanza wakaitwa “Wakristo” kisha nabii akaja katika Yerusalemu na akatangaza kuwa kutakuwa na njaa kubwa. Kwa hiyo wanafunzi katika Antiokia wakaamua kutuma pesa katika kanisa la Yuda ikiwa ni pamoja na Sauli na Barnaba kuwasaidia katika kipindi hicho.

Baada ya hili, Herode, mfalme wa Palestina (au eneo la Israeli) akaanza kulitesa kanisa. Akamwua Yakobo ndugu yake na Yohana kwa upanga na akamweka Petro katika kifungo. Haya yote yalifanyika ili kuwafurahisha Wayahudi. Kanisa likaomba kwa ajili ya Petro. Katikati ya usiku kabla ya kuletwa kwa Wayahudi malaika wa Bwana akaja na kumchukua kutoka kifungoni. Petro akafikiri alikuwa katika maono na hakutambua kwamba yote yaliyokuwa yanatendeka yalikuwa kweli mpaka alipokuwa huru. Petro akaenda katika nyumba ya Mariamu, mama yake na Yohana Marko. Msichana akasikia alipogonga mlango lakini akafurahi mno alipomwona Petro kiasi kwamba akasahau hata kumkaribisha ndani.
Kwa hiyo akaendelea kugonga. Kisha waumini wengine waliokuwepo pale wakasikia na kumkaribisha, akawanyamazisha kimya na kuwaomba wawaambie wanafunzi wengine kuwa yuko huru. Kisha hakukawia akaondoka na kwenda sehemu nyingine.

Herode akakasirishwa sana na kutoka kwa Petro gerezani pamoja na kuuwawa kwa walinzi. Baadaye Herode akakabiliwa na tatizo na miji ya jirani. Wakajadili kuleta amani na wao na wakati wa sherehe Herode akaanza kuongea na watu wakamsifu kama mungu. Malaika wa Bwana akampiga kwa sababu hakumpa Mungu utukufu, lakini alichukua sifa yeye mwenyewe. Hatimaye Herode aliweza kuliwa na minyoo na akafa.

Hata katikati ya majaribu haya mengi, Neno la Mungu lilizidi kuenea, Sauli pamoja na Barnaba wakaenda Antiokia kutoka Yerusalemu kanisa la Antiokia, kwa maombi mengi ya kufunga, wakawateua Sauli na Barnaba kwenda safari ya Kimisionari.

Maswali ya ufahamu:-

1. Kornelio alikuwa nani?
2. Ni ndoto gani ambayo Mungu alimpa Petro?
3. Kwa nini Petro alikuwa na wakati mgumu katika kwenda kumtembelea Kornelio?
4. Nini kilitokea wakati Petro alipofika nyumbani kwa Kornelio na kuhubiri injili?
5. Nini kilitokea wakati Wayahudi kule Yerusalemu waliposikia juu ya hili?
6. Ni wapi kwa mara ya kwanza watu waliitwa Wakristo?
7. Nani alikuwa wa kwanza kati ya wale mitume kumi na wawili kuuawa?
8. Ni kwa namna gani Petro alipata kutoka gerezani?
9. Kwa jinsi gani na kwa nini mfalme Herode alikufa?

Ukweli wa kiroho:

1. **Kanisa lako likiendelea kusambaa – ujiandae kupata upinzani (Matendo 11:3).**

Umejifunza katika somo hili kutegemea upinzani kutoka katika ulimwengu. Je, ulijua pia kuwa unaweza kupata upinzani kutoka kwa waumini? Kwa mfano, baadhi ya waumini wa kanisa wanaweza kutaka liendelee kuwa dogo ili kwamba lionekane na wajisikie kama familia tu. baadihi ya washiriki wa kanisa huenda wasitake kuwafikia na injili baadhi ya aina fulani ya watu. Makanisa mengine katika eneo lako (kama uko katika nchi ambamo kuna makanisa mengine) huenda yasitake wewe kuanzisha makanisa karibu na walipo wao au katika miji. Unapopanuka mara kwa mara unaweza kupata upinzani! Ingawa, usisahau kwamba kanisa katika Matendo ya Mitume mara zote lilipanuka katikakati ya upinzani kama huu. Baba yetu wa mbinguni ni mvumilivu akisubiri kwa sababu anataka wote wafikilie toba (2 Petro 3:9). Tunawajibika kwenda zaidi na zaidi ili kwamba wote wasikie na kufanya uamuzi wa kumpokea au kumkataa mwokozi wetu. Upinzani unapokuja, mara zote jikumbushe mwenyewe na wengine kwamba Mungu anataka watu wote waokolewe na waufahamu ukweli (1 Tim 2:3,4).

2. **Kanisa lako linapokua - ujiandae kusaidia makanisa mengine. (Matendo 11: 27–30)**

Kanisa lilianza Yerusalemu. Kisha Bwana akawatawanya waumini kuanzia Uyahudi na Samaria na kisha katika mataifa ya jirani, muda mfupi baada ya hapo, kutokana na ukame mkubwa makanisa ya karibu kutoka nchi za jirani wakaanza kutoa misaada kwa kanisa mama la Yerusalemu kifedha. Wakashiriki walichokuwa nacho kwa sababu waliwapenda ndugu zao katika Kristo.

Tunatakiwa kufanya vivyo hivyo miaka elfu mbili ijayo. Kanisa lako linapokuwa uwe tayari kusaidia makanisa mengine kwa njia tatu zifuatazo: kifedha (fedha iliyochangwa kwa upendo, ikihitajika), kimwili (kanisa jipya laweza kuhitaji watenda kazi wanapojaribu kujiimarisha), kiroho. Unawezaje kusaidia kiroho? Kati ya furaha moja kubwa katika huduma ni kuweza kuridhisha wengine vitu ulivyojifunza kutoka kwa waumini wapya na makanisa ya karibu. Unaweza kusaidia makanisa mapya katika eneo lako kwa mafundisho na malezi. Kuna furaha kubwa katika kuwafundisha wengine na kisha kuwaona wanaenda nje kuvuna mavuno ya roho kwa ajili ya ufalme wa Mungu.

3. **Kanisa lako linapokuwa – ujiandae kwenda katika utamaduni, nchi au watu tofauti na wa kwako**
   (Matendo 10:34 na 13:3)

Ni matumaini ya somo hili kwamba unajifunza masomo haya kwa matumaini ya kuanzisha kanisa. Labda una kikundi kidogo tu cha watu 2,5 au 12 wanaokutana na kuomba kwa ajili ya mambo yaliyoko mbele. Labda una makundi mengi ambayo tayari yanakutana. Labda una kanisa uliloanzisha tayari, lakini unajaribu kulisaidia kuwa na maono makubwa kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Katika hali yoyote uliyonayo tokea mwanzoni lazima ufikiri jinsi kanisa lako litakavyokua na kuzaa kupitia utume (missions). Mungu ametuita kutangaza neno lake katika Yerusalemu, Uyahudi, Samaria na hata katika mwisho wa nchi (Matendo 1:8). Kwa maneno mengine, anakutaka wewe uanzie katika mji wako na kwa wakati huo huo uwe na maono ya jinsi unavyoweza kuifikia na neno miji iliyoko jirani, majimbo na mataifa. Mungu alimchukua Petro na akamwonyesha kuwa yalikuwa mapenzi yake kwamba Petro asiwashuhudie Wayahudi tu, lakini pia watu wa mataifa. Kanisa lako ataliagiza Mungu kumshuhudia nani? Kikundi kipi cha watu kinaishi karibu nawe ambacho ni sehemu ya mpango wa Mungu kwako kukifikia?.

Mungu alimchukua Sauli na Barnaba na wakaanza kazi ambayo ilieneza injili wakati wa maisha yao wakielekea Rumi (Mdo. 27: 16:30), na pengine hata kufika Spania (Warumi 15: 24). Tunapofunga somo hili, tunaona kanisa linafanya amri ya mwisho ya Kristo. Kanisa lilibadilisha mwelekeo na kuanza kuangalia wa mataifa na likaanza kueneza injili duniani kote. Kanisa la Antiokia likamtua Sauli (au Paulo) na Barnaba katika safari yao ya kwanza kati ya nne za kimisionari.
Kutokana na kazi iliyofanywa na wanafunzi hawa wa kwanza kanisa likasambaa hata mbali ya mipaka ya Yerusalemu. Lilisambaa mpaka likafika katika nchi yako na hatimaye katika nyumba yako.

Mshukuru Mungu kwamba aliileta kweli katika masikio yako. mshukuru Mungu kwamba alikileta kikundi chako cha waumini pamoja. Hata kama kikundi chako ni kidogo, au kikubwa, tajiri au maskini, Mungu anataka kukutumia kama kanisa. Isitoshe ukifuata mapenzi yake kwa kuweka maombi kama msingi wa huduma yako pamoja na neno, ukifuata maagizo na yale madhumuni saba ya kanisa: maombi, ushirika, ibada, huduma, kufuasa, uinjilisti na utume, kikundi chako cha waumini, kitakuwa kanisa zuri lenye afya. Mwombe Mungu akuonyeshe ni wapi kanisa lako liende baada ya hatua hii, kuwaleta wengine katika furaha kuu ambayo wewe unayo katika YEYE.
Utukufu na heshima vimwendee Bwana wetu na mwokozi Yesu Kristo.

SOMO 9
Nini kinafuata?

Unapohitimisha somo hili, unaweza kushangaa, “sasa nifanye nini?”
Unaweza kuwa unafikiria kuwa ni jinsi gani sasa utaenda kuwafundisha watu wako baada ya kuwa umekamilisha somo hili? Isitoshe kwa sababu fulani kanisa lako huenda tayari limeanza tokea mwanzoni mwa mpangilio wa uinjilisti wa ki-uvumbuzi. Huenda umetumia masomo ya Biblia yaliyoandikwa kabla pengine kwa wiki 23 zilizopita. Kwa maneno mengine, hiyo ni karibu nusu ya mwaka wa masomo ambao umeandaliwa kwa ajili yako na mtu mwingine. Kwa hiyo ufanye nini sasa?

Lengo mojawapo la masomo haya lilikuwa kukusaidia wewe kukua katika ufahamu wa maandiko. Huenda umesoma Mathayo au Yohana katika masomo ya uinjilisti na kufuasa. Sasa umeangalia katika sehemu ya kwanza ya kitabu cha Matendo. Matumaini yetu ni kwamba sasa una ufahamu wa msingi wa vitabu hivyo, na kwamba umeanza kukua katika kupenda kujisomea maandiko.
Katika masomo haya ya Biblia tunatumaini umegundua kuwa Mungu anatupa mafundisho mengi ya kweli za kiroho, kupitia neno lake. Kwa masomo 23, umekuwa ukipata kweli za kiroho zilizoandikwa na watu wengine, sasa tunadhani tumekusaidia kuweza kupata kweli za kiroho zako mwenyewe kutoka neno lake. Kama uko kama makanisa mengi duniani, hutakuwa na nguvu ya kuendelea kwenda nje na kutafuta masomo ya Biblia yaliyoandaliwa. Unahitaji kuwa na ufahamu na ukweli wako mwenyewe kutoka katika Biblia. Mungu anataka kujifunua kwako kupitia Neno lake. Unaweza kupata kweli za kiroho sehemu yoyote katika Biblia unapotafakari neno lake. Unapoanza kujisomea neno lake ili kupata kweli za kiroho au ufahamu, ushauri wetu leo ni kuwa ujaribu kusoma kitabu chote cha Matendo ya Mitume. Kwa nini Matendo ya Mitume? Tumekuwa tukijisomea kitabu hiki kwa undani, na inaonekana inaleta maana tukimalizia somo tulilolianza.

Hebu tuanze na sura ya kumi na tatu. Kuna kweli kadhaa za kujifunza katika sura hii, lakini ni jinsi gani unapataje kweli za kiroho?

1. Anza na maombi. Mwombe Roho Mtakatifu kuufunua ukweli kwako, isitoshe tumejifunza kwamba ni yeye (Mungu) anayeufunua ukweli (Yohana 16:13).
2. Unapomaliza kuomba, anza kusoma Matendo ya Mitume 13. Ni vizuri kusoma angalau sura kadhaa zinazotangulia sura ya 13 na sura kadhaa baada yake ili kupata wazo zuri la hali na mazingira.
3. Tafakari kile unachokisoma. Usisome kwa haraka tu. unaweza kumaliza para hii kwa muda mfupi tu. ingawa, jaribu kumruhusu Mungu kuongea nawe kuhusu kile ambacho kipo katika neno lake.
4. Mruhusu Bwana aongee nawe kabla ya wewe hujaongea na wengine. Kweli za kiroho zinahitaji kuwa za mtu binafsi. Yanahitaji kuwa ni mawazo ambayo yanaweza kuhusishwa na maisha yako au katika uhai wa maisha ya mwili wa Kristo – (Kanisa). Usisome habari na kusubiri Bwana akuambie kitu fulani juu ya mtu mwingine. Ngoja akuguse maisha yako kwanza na kisha utaweza kufundisha

kwa bidii ya moyo kwa wengine. Unapotafakari mstari fulani na kweli ukagusa moyo wako, huyu anaweza kuwa Roho Mtakatifu akijaribu kukufundisha.

5. Unapotafakari mistari unaweza kuwepo mstari mmoja, au habari moja, ambayo hasa inakugusa. Kwa sababu fulani, mstari huu utauona kwa upya. Inawezekana umeisoma habari hiyo hata safari 20, lakini leo unahitaji kuzama zaidi katika mstari huo mmoja. Katika "Kanisa ni nini?" mbali na kweli za kiroho unaweza kuona sura na mstari ambapo tulipata kweli ya kiroho. Mistari hiyo iligusa mioyo yetu. Ingawaje, lazima usome tena sura hizo na ugundue kweli za kiroho katika mistari mengine ambazo zinalenga maisha yako mwenyewe.
6. Tulia. Mwombe Mungu akusaidie kuhusisha mstari huo au sehemu katika maisha yako. Fikiri kuhusu kile kilichotokea katika mstari huo na uangalie ambacho wewe au kanisa lako linapitia ambacho kinaweza kufanana na hali hiyo. Au, tazama ni nini mstari huo unakufundisha kuhusu Baba wa mbinguni ambacho hapo mwanzo ulikuwa hujakifirikia, chukua muda. Hakuna sheria kwamba lazima umalize Matendo 13 yote. Inawezekana kuna kweli za kutosha katika habari hiyo kwa kanisa lako kujisomea kwa wiki nyingi. Mimi binafsi niligundua kweli zingine zaidi katika maisha yangu katika Matendo 13:44 na 13:51. Mungu anaweza kuwa na kweli za kiroho tofauti kabisa kwa ajili yako.
7. Hakikisha - kama wewe ni mpya katika imani au katika Biblia kuhakikisha kweli zako za kiroho na maandiko mengine inaweza kuwa ni vigumu sana. Ingawa, unatakiwa kuhakikisha kwamba kile ulichojifunza kimsingi kinakubaliana na kile ambacho Biblia inasema.
   Isitoshe, unaweza kuchukua mstari wowote katika maandiko na kuufafanua vyovyote utakavyo. Mungu hatakuambia kufanya kitu ambacho moja kwa moja kinapingana na neno lake. Soma sehemu zingine za maandiko kuhakikisha kuwa unatoa mafundisho ya kweli. Hii itakuwa rahisi ikiwa utajenga tabia ya kuwa na muda kwa ajili ya neno.
8. Husisha – Baada ya kupata kweli za kiroho na kuzihakikisha katika maandiko, sasa unaweza kuzihusisha na mioyo ya watu wako pamoja na wewe. Jaribu kutafuta mifano na vielelezo ambavyo vinakubaliana na ukweli huu. Watu wako hawatajifunza kitu vinginevyo wanaelewa jinsi ukweli huu unavyohusika na maisha yao.
9. Funga kwa maombi – mara zote mshukuru Mungu kwa yale yote aliyokuonyesha na omba msaada wake unavyowaonyesha watu wako kile ulichojifunza.

KAMWE USISAHAU KUMWOMBA AKUSAIDIE KUWAFUNDISHA WENGINE KUFANYA KITU KILE KILE KATIKA MAISHA YAO.

Kumbuka Mungu anakutaka kuinua viongozi zaidi kwa ajili ya ufalme wake. Kutakuwa na wanaume na wanawake wengi katika kanisa lako ambao unaweza kuwafundisha kulisoma neno ili hatimaye nao wawafundishe wengine.

Unaweza kutumia mawazo haya juu kila siku kupata kweli za kiroho kutoka katika Biblia. Ukitumia mawazo haya ukiwa katika muda wa ibada ya kila siku (devotion) na Baba, kamwe hutategemea tena mafundisho ya Biblia ya kuandikwa kabla. Bila shaka utatumia mafundisho ya wengine ya Biblia muda baada ya muda, lakini kamwwe HUTAYAEGEMEA KAMA NDIYO MSINGI WAKO kwa ajili ya kanisa lako. Kitabu

pekee ambacho utahitaji kiongoze kanisa lako ni Biblia. Acha akufundishe kila siku, ili kwamba uweze kuwafundisha wengine.

> Bwana akubariki unapoanzisha kanisa lako au hata kama unaanzisha makanisa mengi, yawe makanisa yaliyosimama na kwamba yanaongozwa na Roho, yakijengwa katika Biblia na maombi, yakitimiza maagizo ya ubatizo na ushirika Mtakatifu na kutimiza yale makusudi saba ya kanisa – maombi, ushirika, ibada, kuhudumu, kufuasa, uinjili